# Kutoka Kwa Tatu

Jeffersonville, Indiana, Amerika
Juni 30, 1963

1 Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya neno la maombi. Tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, sijui kama kuna ombi maalumu ambalo lingehitaji kujulikana mbele za Mungu, inua tu mkono, na shikilia tu hitaji lako chini ya mkono wako.

2 Baba wa Mbinguni, tuna shukrani kwa ajili ya huu wakati mwingine kukusanyika pamoja upande huu wa Umilele. Tunatafuta nguvu upya kutoka kwako asubuhi hii zitupe ujasiri kwa ajili ya safari iliyoko mbele yetu.

Tumekusanyika kama walivyofanya wana wa Israeli kila asubuhi na mapema, ili wapate mana ile waliyopewa usiku iwasaidie katika siku inayofuata. Tunakusanyika kwa ajili ya Mana ya kiroho asubuhi hii ili itupe nguvu kwa ajili ya safari.

3 Chini ya ile mikono iliyoinuka, Unajua yale yote wanayohitaji, Bwana. Na naomba maombi yangu pamoja na yao mbele Yako, kwamba Wewe utawapa kila hitaji wanalohitaji. Waponye walio wagonjwa na wanaoteseka, Bwana. Tunajua Wewe ndiwe Mungu, na unaweza kufanya mambo yote na uliahidi kuyafanya, ikiwa tutafanya tu kama wimbo ulivyotuagiza, Amini tu; na kama tulivyosikia maneno ya utukufu. *Tembea na Uzungumze na Mfalme*

Sasa, Baba Mungu, bariki Neno Lako linapopita asubuhi hii, na liweze kupata pa kupumzika mioyoni mwetu, kwamba liweze kuleta yale mambo tunayoomba, Baba. Tunaomba katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi. Asante, dada.

Naamini ilisemwa, "Nalifurahi waliponiambia twende Nyumbani kwa Bwana."

4 Tulipokuwa tukiondoka Hot Springs jana, Ndugu Moore alikuwa akisema, "Ndugu Branham. kwa nini husafiri kwenda chini kule Texas ... , pamoja na mimi, kwenye mkutano chini kule? Upumzike kwa siku kadhaa?"

Nikasema, "Nina ibada mbili kesho."

Akasema. "Ibada mbili?"

Nikasema ... Ndiyo ...

Akasema, "Kwa jinsi ulivyohubiri kwa nguvu hapa. mtu anapaswa kupumzika wiki moja kila baada ya kila moja. Mchukulie rnchungaji, atatoa ujumbe wake wa Jumapili asubuhi na kadhalika, halafu anapumzika siku zilizosalia za wiki. Na hivyo... labda itachukua kama dakika thelathini hivi. Unahubiri hapa kwenye masaa mawili au matatu kwa wakati mmoja, ndipo, siku baada ya siku na wakati mwingine mara mbili kwa siku na ndipo unahudumia mstari wa maombi, huko kutambua siri za mioyo kote." Akasema, "Sasa, unasema unakwenda nyumbani na kuwa na ibada mbili Jumapili?"

Nikasema, "Ndiyo, bwana."

Akasema, "Unalifanyaje hilo?"

Nikasema, "Msaada wangu hutoka kwa Bwana," unaona

"Wakati umekwenda," kama mmoja-mtu mmoja alisema muda mfupi uliopita katika maombi, nilipoingia tu .. Wakati umekwenda na hitaji ni kubwa, na tupo hapa kujaribu kuweka sehemu yetu ndani ili kusaidia huu wakati mkuu tulionao.

5 Sasa, Bwana akipenda, usiku huu, nataka kuhubiri juu ya somo: Je, Maisha Yako Yanastahili Injili? Nataka nilirekodi hilo kwenye kanda. Sasa, sijui kama watalirekodi hili kwenye kanda asubuhi hii au la; awaona wengine chumbani. Kuna baadhi ya watu mle ndani-nadhani wapo mle.

Nilifikiri Ndugu Neville angelifanya hili. Nilimhitaji Jumapili iliyopita, kuwa, aweze kuendelea na ujumbe wake, na ndipo aendelee na aniruhusu tu niingie na kitu fulani nyuma yake. Lakini, kama wanataka kulirekodi somo la shule ya Jumapili, mbona, itakuwa vyema.

6 Ndipo, Bwana, akipenda, Jumapili ijayo, hiyo ni kama Bwana ataruhusu, na tuwe hapa, nataka kuzungumza juu ya lile somo nililokuwa nikitaka kwa muda mrefu, na

niliahidi nitahubiri -jumbe kama hizo katika hili hekalu kwanza, zile jumbe zilizorekodiwa. Nataka kukishtaki hiki kizazi kwa ajili ya kumsulubisha Yesu Kristo, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda. Sasa, usiku huu, kwenye saa moja au saa moja na nusu ni ujumbe wa Je Maisha Yako Yanastahili?

7 Sasa, wakati ninaponena juu ya jumbe kama hizo, nasema mambo ambayo yanakata hasa. Silimaanishi hasa kwa ajili ya hili kanisa hapa, au kitu fulani. Mnakumbuka, ninapohubiri, hilo linakwenda duniani kote. Tuna kanda zilizorekodiwa ulimwenguni kote; na wanachukua hizi jumbe huko nyikani na kila mahali. Na Roho Mtakatifu wakati mwingine huniongoza kusema jambo fulani ambalo linaweza kuwa jambo hasa lile Yeye analotaka kwa ajili ya mtu fulani kule Australia au mahali fulani au kitu fulani.

Kwa hiyo labda katika hali fulani ungelisema, "Vema sasa, hiyo hali haipo hapa. Nina hakika ninyi watu mnalielewa hilo.

Sasa, hizi jumbe hazielekezwi kwa yeyote-zinaelekezwa tu kwa Kanisa kwa ujumla, kila mahali; chochote kile Bwana atakachotuongoza kusema na kufanya.

8 Tulikuwa na wakati mzuri sana kule Hot Springs, kwenye mkutano wa Kipentekoste wa mtindo wa kale. Nina hakika wengi wenu mnaridhika ninyi mlio watu wa Pentekoste chini kule kwenye mkutano; ninyi, mliokwenda kule. Vema, sijui lile kundi; nilipaswa tu kwenda kule chini kwa wiki moja, na niliwapa siku mbili au tatu. Lakini nataka kusema jambo moja, katika ule mkutano hakika walikuwa na imani ya kuamini. Kama yeyote miongoni mwenu angekuwa pale…Ambapo najua huyu mama hapa, alieyeketi kwenye kona-sijui yeye ni nani, au hapa hapa, najua yeye alikuwa kule. Na najua baadhi ya ndugu walikuwa kule, Ndugu Jackson na wengine, Ndugu Palmer.

9 Hicho ndicho watu hupata wanapokuwa na imani, unaona. Unaona ule ni mstari wa maombi? Hakukuwa na mmoja aliyeingia au kutoka, ila yule aliyeponywa na Mungu. Unaona? Unaona?

Kwa hiyo unapokuwa na imani ...Na jambo lingine, inawezekana kuna baadhi yenu, wasioweza kuelewa ule msisimko-kucheza, kupiga kelele. Vema, wao tu-hawamtazami mtu fulani yeyote; wanapiga kelele tu mbele za Mungu. Mnaona? Sawa.

Lakini, nataka kusema, ndio-wanawake wanaoonekana wasafi zaidi niliowahi kuwaona-hizo nywele ndefu. Na watu kutoka kule nyikani, kule vichakani, lakini siamini kama niliona mtu yeyote kote aliyeonekana wa namna ya kisasa zaidi (mnajua ninachokimaanisha) kwa namna zote za kujipodoa na mapambo. Naweza nisikubaliane nao katika yote wanayofundisha, lakini hakika naweza kukubaliana nao katika hilo. Hao walionekana kama Wakristo kwangu.

10 Hivyo, Bwana aliniongoza kuhubiri juu ya somo, jana au juzi adhuhuri, *Mara Moja tu Zaidi, Bwana*. Na kama kanisa, baadhi yao pale hawakujua nilifanya hilo kwa kusudi, kwa sababu Bwana aliniongoza kufanya hivyo. Lile kundi dogo lilikuwa linapotoka katika jambo fulani; na Bwana alisaidia kwa ajili ya hilo ili kulifanya hilo.

Kwa hiyo, lilikuwa zuri tu. Hakika... Mnajua mambo huendelea, kama huna jicho la kiroho, huelewi. Unapaswa kutazama mbele kwenye hayo mambo.

11 Niliingia ndani, na huyu Ndugu Ungren-hiyo ni kwenye mara ya pili kumsikia huyu mtu akiimba. Nilipokuwa nikiingia tu chumbani, alikuwa anaimba, *Natembea Na Nasema Na Mfalme*. Nikawaza, "Je, hilo si jambo zuri mno?" Jinsi ambavyo Mfalme-ameonekana akitembea na kusema, hiyo inamaanisha ushirika wa kudumu. Siyo tu katika kanisa, ila kila mahali, tembea na sema na Yule Mfalme.

12 Na pale-tazameni juu ukutani. Kulikuwa na kadi iliyoshikiliwa kwenye picha ndogo ndani pale ya tukio fulani ambayo mtu aliyeitwa George Todd alikuwa amenichorea. Sijui kwa nini yule mtu alilifanya hilo, labda huenda, hakuwaza tu; na alikuwa ameichora, na ni picha ya upande wa nyuma wa mlima msituni na kijito kikitoa mawimbi, na ule upande mwingine wa kijito kumesimama kulungu jike na mtoto wake .masikio yao yakiwa yamesimama, wakitazama ng'ambo ya kile kijito. Sijui kama bwana Todd yupo hapa, simfahamu. Lakini, nataka kusema hili, Bwana alisema na mimi nilipoitazama ile picha; na labda yeye hakujua alipokuwa anaichora.

Mnakumbuka hadithi yangu fupi kuhusu kulungu ambaye yule mtu alikuwa ampige risasi ... Vema, yupo hapo pamoja na mtoto wake, kando ya maji ya uzima, unaona.

Uvuvio, jinsi gani yule mama kulungu na mtoto wake walikuwa pale, na nikawaza, ndiyo, na ule upande mwingine ambapo kuna-kando ya miti mibichi. Niliona mama na mtoto pale pia, wakisubiri pale.

Asante, Ndugu, Ndugu George Todd, kama huyo mtu yupo hapa asubuhi hii.

13 Sasa, ningalikuwa na somo la shule ya JumapiIi, mara nyingi huwa nalirefusha. Ni kitu ambacho huwa kinanisukuma moyoni mwangu, sijui, tangu jana-sasa tu-kama Bwana-ni somo. Ninazeeka, na sijui ni muda kiasi gani zaidi nitakuwa hapa.

Lakini, kuna swali kubwa katika kanisa linalofanya watu wahitilafiane na kuwa na mawazo tofauti. Kama tu kule kuliwa kwa tofaa, na nilihubiri kwenye ujumbe, na naamini kwa dhati naweza kulithibitisha kwa Maandiko kuwa hayakuwa matofaa, unaona-ilisababisha kuchanganyikiwa kwingi.

14 Kwa hiyo labda kabla hatujaondoka-inatubidi kurudi nyuma sasa, kwenye siku thelathini, unajua-nyuma kule Arizona. Kwa hiyo kabla sijaondoka, Bwana akipenda, ningalipenda kuchukua hili Andiko, na bila kulirekodi. Kama mkilirekodi, msiuze hiyo kanda-msiruhusu isambazwe. Nataka kuelezea Ukweli halisi wa ndoa na talaka. Ni swali na hizi ni nyakati za mwisho, ambapo mafumbo yote ya Mungu yangetimizwa.

Jana, nilipokuwa nikija nikikatisha milimani mchana, Roho Mtakatifu alionekana kusema na mimi, "Rekodi hilo na ulihifadhi mahali."

Sijui ni kwa nini; lakini, "Ukweli halisi wa ndoa na talaka." Baadhi yao husema, "Watu wanaweza kuoana kama wanaweza kuapa kuwa walikuwa kwenye uzinzi," na wengine husema, "Vema, kama wakitendeana vibaya na hawawezi kuishi pamoja." Ni bora kuishi duniani katika amani, kuliko kuishi jehanamu duniani" -hayo maswali yote tofauti na wengine huwaoza kwa njia yeyote ya zamani. Baadhi hutaka kunyunyiza maji matakatifu juu yao, na kuwageuza nyuma na kusema hawakuwahi kamwe kuoana, wanawabariki, na kuwageuza tena mbele kukabili kanisa. Kuna namna zote za mchafuko. Lakini kama kuna mchafuko kiasi hicho, kuna Ukweli mahali fulani.

Naamini, na kulisema hili kwa unyenyekevu: naamini Bwana amelifunua kwangu, na-ile Kweli, Na kama lingalifika miongoni mwa makanisa, lingeyararua vipande vipande, ambapo labda inabidi kuwa hivyo. Lakini, ni ... ni heri ningeliwaacha wachungaji-niwaache tu-wachungaji wa yale makanisa wapate kanda, ndipo wazicheze na halafu waweze kuongoza kuanzia pale na kuendelea. Lakini, ningelipata kurekodi lile tu ili kuonyesha Kweli yake halisi.

Naamini huu ni wakati ambapo mafumbo haya yatatimizwa, yatakwisha. Wameduwaa kama tulivyosema kupitia nyakati za kanda tulipokuwa tukileta ile *Mihuri Saba* na *Vipindi Saba Vya Kanisa*.

15 Na sasa tunakabiliana na wakati wa *Baragumu Saba* na ndipo vile *Vitasa*. Na labda tungaliweka mkutano wa wiki moja na kuyaweka yote pamoja. Ningalipenda lirekodiwe.

Na ndipo mbali na hilo, najaribu sasa kulifanya lisomwe kuondoa makosa na kutengeneza vitabu juu yake, Vipindi vya Kanisa, vitabu saba vya *Vipindi vya Kanisa*, kanda saba, na kuviweka vifanyike kwa bei ya chini tuwezavyo, ili kila mtu aweze kuvipata.

Ndipo, kama Bwana atakawia kuja, na niendelee kuishi, mtaona kuwa yale mambo niliyosema katika Jina la Bwana yatakuwa-yatatukia kama yalivyosemwa. Hayakuwahi kushindwa bado, na baadhi yake yatatokea baadaye.

16 Na mimi, natumaini kuwa Bwana atatuhusu kufanya hilo moja kwa moja. Tutawataarifu watu, muda, kwa sababu kuna wengi;wanaopenda kuja na kusikia hayo mambo, na nashukuru kwa hilo.

17 Kama hakuna mtu aliyeliamini au aliyelisikiliza, ingenifaa nini kusimama hapa na kuserna chochote kuhusu hilo? Unaona. Ningalikuwa kama ninayetupa mkate juu ya maji, utakuwa kama ... Kama hakuna anayekwenda kuliamini, basi itakuwa kama kutupa lulu mbele ya nguruwe. Lakini kuna maelfu mara maelfu wanaoliamini hilo, na wanashikiliakila neno, na tungependa kuwaingiza wengi kwenye ukumbi iwezekanavyo wakati tu-tutakapokuwa tayari kuwa na hizi ibada na kwa ajili ya utukufu wa Bwana. Na tunatumaini kuwa Mungu atatupa hilo. Na sitaki kuwa na hilo, hadi niwe nimevuviwa Kiungu kulifanya hilo.

Mungu ana wakati kwa ajili ya kila kitu, unaona. Hupaswi kutangulia mbele yake.

Kama ukivuna ngano yako kabla-ukiweka mashine ya kuvuna kabla ngano haijaiva, utapoteza sehemu kubwa ya ngano yako, unaona. Kwa hiyo, mundu unapokuwa tayari kutupwa ndani, Mungu atautupa ndani. Ndipo tutakwenda kuvuna. Lakini na…

18 Ninaposhinikizwa namna hiyo, nilifikiri ningejitoa katika hilo kwa muda mfupi. Siku nzima ya jana, sikuweza kuliondoa mawazoni mwangu na usiku mzima wa jana. Nilikwenda kulala kwenye saa sita usiku, nikawa na kama usingizi wa masaa matatu usiku wa juzi, na usiku wa jana sikuweza kulala, hata hivyo. Kitu fulani kilisema, "Rekodi ile *Ndoa Na Talaka*," unaona.

Bwana akipenda, kama hilo litaendelea moyoni mwangu na Bwana akanionyesha mengi zaidi kuhusu hilo, vema basi, naweza kulirekodi hilo, unaona.

Lakini kumbukeni, kwa ajili ya wachungaji tu. Mje, lakini msikilize, Iakini kanda yenyewe, hebu ... Unaona, kwa sababu inakwenda miongoni mwa kusanyiko, na baadhi ni *hivi* na wengine ni *vile*, na kuwa na maoni yao wenyewe. Na nataka ndugu wahudumu kuwa na hili katika kujifunza kwao wenyewe, na ndipo waende kutokea hapo, kwa sababu wao ndio wanaowajibika-ndio wanaowajibika.

Ungeweza kwenda na kumfungulia kanda jaji asikilize-baadhi ya hawa wanasheria.

19 Muone kile Bwana alichosema kuhusu hii *Ndoa Na Talaka*. Ni la utukufu zaidi kuliko vile watu wanavyofikiri. Na litachanganyika moja kwa moja na *Uzao Wa Nyoka*. Ni kitu kile kile, kikiendelea tu; hayo ndiyo mafumbo yenyewe.

Mnakumbuka, "Katika siku za Malaika wa Saba, mafumbo yote ya Mungu yatatimizwa," mambo yasiyofahamika ambayo Bwana atayamaliza.

Sasa, kadiri ya...

20 Sasa, kumbukeni... mtaanza mkutano wenu saa moja na nusu, sivyo? Sasa, Ndugu Neville, ama una ujumbe kwa ajili ya usiku huu, hubiri, unaona. Haitanichukua kwenye sasa moja au dakika arobaini na tano, na nitaurekodi wote uliobakia. Napenda kumsikiliza Ndugu Neville. Nampenda. Yeye ni ndugu yangu. na nafikiri yeye ni mhubiri mzuri sana-mhudumu mzuri mno. Na ... jambo moja kuhusu Ndugu Neville nilipendalo, anaposema chochote. anakiishi kile anachokiserna. Sasa, hilo ndilo jambo kuu. Unajua si bora zaidi kumhubiria mtu kwa maisha unayoishi kuliko kumhubiria kwa maneno tu? "Kwani ninyi ni waraka ulioandikwa, ukisomwa na watu wote. "

Sasa, hebu kabla hatu…

21 Hatujaweza kurudisha kurasa nyuma, lakini Mungu inabidi afungue hili somo la Jumapili. Kwa hiyo, hebu tumwombe tu Yeye alifanye hilo.

Baba wa Mbinguni, sisi kwa imani tunatazama wakati ujao. Natazama sasa, kwa imani, kwenye jambo linalokuja, Bwana. juu ya dunia, ambalo litawavuta watu Wako kuwa pamoja.

Tunapoona makanisa ya kidhehebu yakiwabana sana watu na kuwa tofauti, hakika linawatoa watu nje.

Kama tu ilivyokuwa katika Misri. Farao akiinuka, ambaye hakumjua Yusufu. Kama ilivyokuwa katika Ujerurnani na kule Urusi na ltalia. Watu waliinua Josephs. Hitler. Stalin, Mussolini, ambao waliwachukia Wayahudi. Iliwabidi warudi katika nchi yao.

Mungu, Unazo njia za kutendea mambo ambazo hatuzielewi, na uliwashinikiza-Ujerumani siyo nyumbani, waIinyang'anywa kila kitu; pia katika Italia, Urusi-hakukuwa na mahali pa kwenda, na walirudishwa nchini kwao, kutimiza tu Neno.

Loo, mkono wa upendo wa Mungu jinsi gani, wakati mwingine huonekana wa kikatili, jinsi watu wanavyoteseka, lakini bado ni mkono wa huruma wa Yehova, ukiwaongoza watoto Wake wadogo. Tunakushukuru, Bwana.

22 Sasa, naomba, Mungu, ninapoona siku ambayo dhehebu linakandamiza waamini,

likiwatenga, likisema kuwa majina yao lazima yawe katika kitabu chao, vinginevyo wamepotea, hawahusiki na lile kundi lingine. Ni mkono wa huruma pekee wa Yehova, ukiwaongoza-kwenye Mti wa Uzima. Naomba, Bwana, kwamba kila mmoja-najua watafanya, kwa sababu ni Neno Lako, nalo haIiwezi kushindwa. Na tuongozwe kwenye miti wa Uzima, ili tuwe wamiliki wa Uzima wa Milele, tuone mkono wa Mungu, na kwa macho ya imani, tutazame zaidi ya vivuli hivi tunavyotembea ndani yake leo, tuone Nchi

ya Ahadi ikiwa tu mbele yetu.

Bariki Neno Lako asubuhi hii, Bwana, haya Maandiko machache na muhtasari niIioandika hapa. Roho Mtakatifu na aje sasa, ninapojiweka wakfu mimi mwenyewe kutahiriwa ulimi, na mawazo, na akili, na kanisa likiwekwa wakfu masikio yao ya kuelewa, mioyo yao, na sisi sote pamoja, kwamba Utazungumza nasi kupitia Neno Lako, kwani Neno Lako ni kweli. Katika Jina la Neno, Yesu Kristo, tunaomba. Amina

23 Sasa, fungueni Biblia zenu kwenye Kitabu cha Kutoka. Na sasa, nataka kusoma sehemu ya Maandiko kutoka Kutoka, sura ya tatu, kuanzia 1 - 12. Sikilizeni tu kwa makini, tunaposoma. Kutoka sura ya tatu, 1- 12.

*Basi huyu Musa alikuwa akilichunga kundi Ia Yethro mkwewe, kuhani wa Midiani; akaliongoza kundi nyuma ya jangwa, akafika mpaka mlima wa Mungu, hata Horebu.*

*Malaika wa Bwana akamtokea, katika mwali wa moto uliotoka katikati ya kichaka; akatazama, na kumbe, kile kichaka kiliwaka moto, nacho kichaka hakikuteketea,*

*Musa akasema, nitageuka sasa, niyaone maono haya makubwa, na sababu ya kichaka hiki hakiteketei.*

*Bwana alipoona ya kuwa amegeuka ili atazame,*

Nataka kusisitiza juu ya hilo.

*Bwana alipoona ya kuwa amegeuka ili atazame, Mungu akamwita kutoka katikati: ya kite kichaka, akasema, Musa, Musa. Akasema, Mimi hapa.*

*Naye akasema, Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana hapa unaposimama ni nchi takatifu.*

*Tena akasema, Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Musa akaficha uso wake kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu.*

*Bwana akasema, Hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri, nami nimesikia kilio chao kwa sababu ya wasimamizi wao maana nayajua maumivu yao.*

*Nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri. niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema, kisha pana; nchi ijaayo maziwa na asali; hata mahali pa Wakanaani, na Wahiti, ... [na Waamori, na Waperizi] ... na Wahivi, na Wayebusi.*

*Basi, tazama, kilio cha wana wa Israeli kimenifikilia; tena nimeyaona hayo mateso ambayo Wamisri wanawatesa.*

*Haya basi, nitakutuma sasa Kwa Farao...*

24 Mnaona? "Nimeshuka, lakini nitakutuma sasa." Mungu akienda katika umbo la mwanadamu. "Nenda ... " Hebu nisome hii aya ya kumi tena.

*Haya basi, nitakutuma sasa kwa Farao, ili upate kuwatoa watu wangu, hao wana wa Israeli, katika Misri.*

*Musa akamwambia Mungu, Mimi ni nani hata niende kwa Farao nikawatoe Wana wa Israeli watoke Misri?*

*Akasema, bila shaka mimi nitakuwa pamoja nawe; na dalili ya kuwa nimekutuma ndiyo hii; utakapokuwa "Umetoka ... [*Samahani.*] Utakapokuwa umekwisha kuwatoa hao watu katika Misri, mtamwabudu Mungu katika mlima huu.*

Bila kuliona hapo kabla, ila kwa kujisikia uvuvio mkuu wa Roho asubuhi hii, nililipata tu hilo. Mungu akimtuma mtumishi Wake kule, alikokua amekukimbia, Yeye alimpa ishara ya mlima. Sikuwahi kuliona hadi wakati huo. Hii itakuwa Ishara ya Milele kwenu, unaona.

25 Sasa, tutakwenda kuhubiri asubuhi hii, juu ya somo la "Kutoka kwa Pili kwa Watu wa Mungu," au "Kuitwa kwa Watu wa Mungu Watoke." *Kutoka* maana yake, iliyotolewa nje, iliyoitwa nje, iliyochukuliwa kutoka, na nataka kutumia hilo kama somo la Kutoka

kwa Pili kwa Watu wa Mungu. [Ndugu Branham anaupa kichwa, *Kutoka Kwa Tatu*, katika ibada ya jioni-Mh.]

26 Sasa, wamekuwa na kutoka kwingi, lakini nazungumza juu ya ule wakati ambao Mungu aliuita kutoka, kutengana na pale walipokuwa kwa wakati huu.

Mungu hapa anakuwa tayari kutimiza Neno Lake la Ahadi ya Kiungu alilowapa Abrahamu, Isaka, na Yakobo. Miaka, miaka mamia ilikuwa imekwishapita, lakini bado, Mungu kamwe hasahau ahadi Yake. kwa majira, wakati uliokubalika, Mungu siku zote hutimiza ahadi Yake. Kwa hiyo, unaweza kuwa na hakika kuwa kile Mungu. alichoahidi katika Biblia hii, Yeye atakifanya. Hakuna tu haja ya kujaribu kuwaza chochote kile na kusema, "Vema, nabii alikuwa-labda alikosea, au hilo Iisingeweza kutokea katika hii siku."

Ilionekana kama lisilowezekana wakati ule, lisilowezekana kuliko inavyoonekana sasa, lakini Mungu alilifanya hata hivyo, kwa sababu Yeye aliahidi angelifanya hilo. Na tazama jinsi Yeye anavyolifanya kirahisi: "Nimeshuka; nilisikia kilio; nalikumbuka ahadi Yangu, nami nimeshuka chini kulifanya hilo, nami nakutuma. Ulifanye hilo, nitakuwa pamoja nawe; hakika nitakuwa pamoja nawe. Uwepo Wangu kamwe, kamwe haushindwi utakuwa pamoja nawe popote utakapokwenda. Usiogope. Nashuka chini ili kukomboa." Nina hakika akili ya kiroho inalidaka hilo. "Nitakutuma kuleta watu wangu watoke, uwaite watoke nje nami nitakuwa pamoja nawe."

27 Sasa, jinsi gani-jinsi gani tunaweza kupumzika, jinsi gani imani inaweza kushika hilo tumaini pale. Mungu anakwenda kulifanya hilo; Yeye aliliahidi hilo. Haidhuru, hali zikoje, au asemacho yeyote yule, Mungu atalifimya hata hivyo, kwa sababu, Yeye aliahidi kufanya hilo. Na Yeye hulifanya kirahisi kiasi kwamba linapita juu ya ufahamu wa akili zilizoelimika, ambazo zingejaribu kufikiri kuhusu hilo. "Lawezekanaje?" Simaanishi kusema kuwa mtu sasa, mwenye akili imara, elimu nzuri, kwamba yule mtu hawezi kuielewa. Hiyo ni sahihi, vizuri sana ili mradi anatumia hiyo, sio kutoa hoja, ila ule utamaduni alio nao kwa kumwamini Mungu.

Hebu libadilishwe katika urahisi wa kusikiliza kile Mungu alichosema na ukiamini. Basi utamaduni Wake utamsaidia.

Tazama, mtu anapojaribu kutoa hoja kuwa haliwezi kutendeka, basi hilo humpeleka mbali na Mungu, daima wakati wote. Wakati anapojaribu kusikiliza... ufahamu wake mwenyewe, unaona. Kama huelewi na Biblia inasema jambo fulani, liitikie tu, "Amina," liache tu liende namna hiyo.

28 Sasa, badala ya kurejea haya Maandiko, unaweza kuyaandika katika hili somo la Jumapili, lakini ninge-... labda kama ungalipenda kuliangalia... lakini kwanza ninayo mengi sana hapa.

Hebu tu- ... Kabla ya kujua huku kutoka kuma maana gani, nakwenda kufananisha kutoka wakati ule na kutoka sasa. Na angalia, kama haiendi sambamba hasa. Moja ni ya asili na jambo lile lile ambalo Yeye alilifanya katika asili. Anaufananisha tena, (kuleta uhalisi wake) katika kiroho. "Kutoka Kiroho."

29 Inashangaza kuona Neno la Mungu-jinsi gani mtu yeyote angeweza kusema halikuvuviwa. Hii ni kwenye miaka 2800 iliyopita, unajua. Ni jinsi alivyoahidi na kile-Yeye alichofanya, na kukiweka pale kama mfano. Jinsi Yeye afanyavyo kivuli cha jambo fulani kushuhudia kile kilicho halisi. (Nitakwenda kwenye hilo usiku huu kati ya mwezi na jua, Bwana akipenda.)

Lakini kwanza, lazima tupitie upya Mwanzo tuone kwa nini walikuwa kule Misri? Kwa nini watu wa Mungu wangelikuwa nje ya ile nchi? Na hata hivyo Mungu aliahidi hilo pale pale mwanzo alipokuwa na Abrahamu, Isaka na Yakobo, katika Palestina. Mungu aliwapa ile nchi, na kusema, "Ndiyo hii."

Vema, basi kwa nini wale watu wasiwe mahali pale alikowapa Mungu? Hilo ndilo swali la leo, pia. Mungu alitupa Pentekoste. Yeye alitupa Kitabu cha Matendo. Yeye alitupa Roho Mtakatifu Atuonyeshe njia na kutuongoza. Yeye alitupa nchi, na kwa nini tuko nje ya hiyo nchi? Kwa nini lile kanisa kuu la Kikristo leo haliishi tena kama Kitabu cha Matendo, likileta jambo lile lile? Kuna sababu yake.

30 Sote tunajua kuwa tumefilisika na tuko katika hali ya kutisha; na hali ya kutisha kuliko zote ambazo Ukristo umewahi kuishi ndani yake ni leo. Na tuko kwenye-moja kwa

moja kwenye ukingo au karibu kabisa na hukumu kuu ya kutisha kwa ajlli ya kanisa, na kabla ya hii hukumu kutokea, Mungu anaita kutoka kama tu Yeye alivyofanya wakati ule.

Dhambi za Waamori zilikuwa zimelundikana. Kwa hiyo Yeye anaita kutoka kiroho. Sasa, hebu turudi nyuma kwa muda mfupi na tufananishe na tujue.

Wao walikwenda Misri kwa sababu tu ya kumwonea ndugu. Hiyo ndiyo sababu ambayo Israeli walikuwa katika Misri kwa wakati ule, nje ya ile nchi. Kumbukeni, ahadi za Mungu zilikuwa tu pale ambapo walikaa katika ile nchi.

31 Sasa, unaweza kuona kile tulichokuwa tukisema katika maombi kitambo kidogo kilichopita? Kwa nini ilimpasa Mungu aufanye moyo wa farao kuwa mgumu? Kuwarudisha wale watu katika nchi.ya ahadi kabla Yeye hajawabariki, ili kuwaletea Masihi.

Jinsi gani aliufanya moyo wa Hitler kuwa mgumu awe dhidi ya Wayahudi, wakati yeye mwenyewe alikuwa nusu Myahudi? Jinsi gani alifanya hilo katika Stalin, Mussolini?

Unaona, watu ambao hawajavuviwa, kama taifa, wao... Mungu inabidi achukue vitu ambavyo wanaishi navyo, mara nyingine ile sheria za nchi, ili afanye ahadi Zake zitokee kweli.

Kwa Hiyo, Yeye ilibidi afanye mioyo ya wale watawala wa mabavu iwe migumu ili kuwarudisha Wayahudi kwenye nchi ya ahadi. Ilipasa iwe hivyo.

32 Sasa, tunakuta kuwa tukirudi nyuma, Yusufu... Tunaijua habari unaporudi katika kitabu cha Mwanzo, na unaweza tu kuIisoma kwa sababu, nimechelewa tu kidogo kuanza juu ya hili somo refu la shule ya Jumapili. Nitajaribu kuharakisha.

Tazama, sasa, soma ile habari ya Yusufu ukiweza, akiwa amezaliwa mwishoni mwa ndugu zake, wa pili kutoka mwisho. Akili ya kiroho italidaka hilo sasa hivi. Yeye hakuwa mtoto wa mwisho; lakini katika kutengwa, tazama. Yusufu na Benyamini walikuwa ndugu wa damu kabisa, na ni hao wawili pekee waliokuwa ndugu.

Benyamini hakuwahi kutambulika hadi alipokutana na Yusufu. Na zaidi ya hao wengine wote, Benyamini alipewa maradufu kwa kila kitu Yusufu alichotoa.

Vema, tazama sasa, tunakuta kwamba chini kule, kulikuwa na…

33 Yeye aliondolewa toka kwa kaka zake kwa sababu yeye alikuwa wa kiroho. Yeye alikuwa mtu mkuu, ingawa yeye alikuwa mnyenyekevu kuliko wote katika kundi lile, mdogo kuliko wote katika lile kundi, na walimchukia bila sababu. Wasingepaswa wamchukie. Wangepaswa wamheshimu, kwa sababu... kwa nini walimchukia? Kwa sababu alikuwa ndugu? Sio hilo hasa. Walimchukia kwa sababu Mungu alijihusisha naye zaidi kuliko Yeye alivyokuwa kwa wale wengine wote.

Mungu alimpa ufahamu wa kiroho. Yeye aliweza kufasiri ndoto kwa usahihi, naye aliweza kutabiri mambo kabla ambayo yalitukia kwa usahihi, kama tu hasa yalivyokuwa-hakujitapa hata kidogo.

Yeye aliota ndoto ya yale masuke yakipiga magoti mbele ya suke lake, nao ndugu zake wakamkasirikia. Wakasema, nadhani basi... "Wewe mtakatifu mdogo anayejiviringisha." Kwa maneno mengine, "Tutakupigia magoti siku moja."

Lakini hivyo ndivyo ilivyotokea. Jinsi gani yale majitu makubwa yangepiga magoti mbele ya mtu mdogo mnyonge aIiyesimama pale, lakini walifanya hivyo. Hakika walifanya hivyo, na kuomba rehema.

Lakini bado hakuwa katika mamlaka, unaona. Wakati ule alikuwa tu katika hali ya kitoto.

34 Na ndipo tunakuta kwa kufanya hili, Yusufu alichukuliwa toka miongoni mwa ndugu zake, madhehebu na akakaa mahali yeye mwenyewe-kaka zake wote katika nchi.

Ndipo kunakuja jambo kuu. Tunatambua kuwa Israeli, ili mradi walikaa katika makao yao na kudumu-sasa hilo ni jambo moja zuri kukaa mahali ulipowekwa, hiyo ni sahihi, lakini walimwacha Roho.

Walio walokole leo, kwa usahihi wanajua kile walicho kwa kuelewa Biblia kiakili, lakini hakuna Roho. Wamemkataa Yusufu, wakamtoa nje. Hawakutaka chochote kuhusu huyo, kundi la watakatifu wanaojiviringisha; ni... Hatutaki chochote kuhusu Roho.

Wamemtenga na ushirika, wakamwuza kwa ulimwengu. Walikuwa nje ya ushirika wao.

35 Sasa, kwa kufanya hilo, waliondolewa mahali pao, wakapelekwa Misri baadaye. Sasa, habari ya hawa ndugu wenye wivu ni mlingano mkuu bila shaka na upande wake wa kiroho leo.

Sote tunatambua hilo, kwamba ni wivu mtupu, wivu mchafu, unaona. Hakuna usafi katika wivu, unaona si chochote ila wivu mchafu.

Wanapoona Biblia ile ile na asili ya Mungu yule yule aliyeandika Biblia, akijithibitisha Mwenyewe na ndipo wanalikataa hilo bila sababu, safi ... vema, safi kama nilivyosema, ni wivu wenye takataka. Wakitazama Mungu akiponya wagonjwa, akifufua wafu. Mungu yule yule aliyeishi katika siku za mitume. lnjili ile ile waliyoiandika kwa ajili ya hii safari ya kiroho. Ni Mungu yule yule anayefanya mambo yale yale, hadi hakuna chochote ila wivu; ametenga na ushirika, na "hatutakuwa nalo hili miongoni mwa watu wetu, " unaona, wanawafukuza.

36 Walifikiri-wale ndugu, kwamba kamwe wasingekuwa na haja na mtu kama yule, kwa hiyo, "Kwa nini asiondolewe." Hilo ndilo... jambo lile lile limetokea leo. Wanafikiri kuwa kwa sababu makanisa yetu yamekuwa ya kiakili, kwamba tuna makundi yaliyovaa vizuri zaidi, mashirika makubwa kuliko yote, zaidi... wachungaji werevu kupita wote, kwamba hatuna haja na Roho Mtakatifu kama ambavyo ilikuwa kule nyuma.

Kwamba wametosheka, kwa maneno mengine matendo hupiga kelele kuliko maneno, kwamba seminari zao na-bongo zao za asili na kujikusanya kwao pamoja na kujadili hili jambo, wanaweza zaidi kwa akili zao wenyewe kuweka kanisa katika utaratibu ulio bora kuliko ambavyo Roho Mtakatifu angeweza kufanya; kwa hiyo hawamhitaji tena. Ni kitu ambacho hatukihitaji leo.

Ni kwamba...siku za hilo zimekwishapita, Sasa, hilo siyo sahihi? "Hatumhitaji Roho Mtakatifu kuponya wagonjwa, tunao madaktari. Hatuhitaji Roho Mtakatifu kunena kwa lugha, sisi sote tu watu wenye akili nyingi." Na unapofanya hivyo, unaondoa kamba ya tegemeo la uzima toka kwenye muundo wa maisha yako.

Yesu katika siku Yake aliwaambia Wayahudi, "Hamkusoma kwamba lile Jiwe lililokataliwa limekuwa Jiwe Kuu la Pembeni, lile ambalo jengo lote linakaa juu yake?"

37 Sasa, mnaona ninalomaanisha? Nina hakika mnaweza kulipata hilo. Kwamba-sababu yake sasa, ni kwa sababu walifikiri kwamba kamwe wasingemhitaji, "Hatuwahitaji wanenaji kwa lugha. Hatuwahitaji wafasiri wa lugha. Hatuhitaji tena manabii wa Agano la Kale kutuweka katika utaratibu kwa Roho Mtakatifu. "Tunalielewa hilo."

Unaona, wamechagua mfumo uliofanywa na mwandamu kuchukua mahali pa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, kuna watu waliochaguliwa, wanayo majina yao kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo; hawawezi kulipokea hilo. Wana akili za kiroho-kwa hiyo, hawawezi kulipokea hilo. Hawawezi kulivumilia. Haidhuru kama baba na mama zao wameishi katika shirika gani la dini au kanisa.

38 Wakati kanisa linapotengeneza au kufanya... labda lisingesema hilo kwa usahihi.

Loo, hapana, wasingetamka hilo kwa usahihi lakini matendo yao yanalithibitisha. Hapa kuna Neno, na Roho Mtakatifu analithibitisha miongoni mwa wale wakati Yeye anapowakusanya pamoja, kwamba Yeye bado anaponya wagonjwa, anafufua wafu, ananena kwa lugha, na kutoa pepo. Kwa hiyo, inategemea kile kilichoko ndani ya mtu.

39 Bi Arganbright, pale, alikuwa anawaza hilo jana, akiwa amekaa pale kwenye matembezi akivuta nyasi-alipokuwa akikata majani bustanini. Nilipita pale pale pembeni mwake, naye hakujua, na nikamwacha tu aendelee. Nilikuwa natazama.

Sasa, tazama, Roho Mtakatifu na kazi Zake kuu.

40 Kanisa linajisikia kuwa halihitaji Roho Mtakatifu. Makanisa yatakuambia hivyo. Na mtu anaweza kusimama na kukupa maongezi ya kiakili na nusura akufanye uamini hilo. Sasa, hebu tusimame hapo kwa dakika moja.

Je, Yesu hakusema kuwa hawa wawili watafanana sana na ingewadanganya wateule halisi kama ingeliwezekana? Mazungumzo ya kiakili yatakuwa yanavutia sana kwamba yangewadanganya watu... Ni injili, ni mtu ambaye anaweza kushika lile Neno kwa namna ambayo angeweza kumfanya mtu yeyote mwenye akili nyingi, ikiwa tu

unaamini katika akili nyingi, wanamlaani Roho Mtakatifu na kuchukua njia ya binadamu. Tunaona hilo.

41 Sasa, hilo ndilo jambo lile lile walilowaza kuhusu Yusufu, nao wakamwondoa. Na kote katika Misri... ee jinsi gani tunaweza kuwaza ... jinsi gani ningetumia masaa... Ungeweza kukaa hapa kwa miaka mitatu na kamwe usingeacha hilo soma, mchana na usiku, na bado uendelee kupata viini vikuu vya Roho Mtakatifu.

42 Akili za kiroho zinaweza kutazama kule Misri na kuona kuwa mateso yanakuja, zinaweza kuona Yusufu akichukuliwa ili kwamba mateso yaje. Na ndipo uone Mungu na gurudumu lake ndani ya gurudumu-kila kitu kikienda kikamilifu tu. Mtazame Potifa akimkataa Yusufu. Tazama ule uongo ukisemwa na uone Yusufu magereza na ndevu zake zilizorefuka, akiwa ametengwa na ndugu zake, lakini ghafla, Mungu akaingilia kati!

43 Jinsi gani tunaweza kuona liIe gurudumu ndani ya gurudumu likitembea-mpango mkuu wa Mungu ukiendelea kila kitu hadi kufikia huku kutoka, hadi wakati huu Yeye anapoita watu Wake warudi katika nchi tena, warejee katika mahali pao, katika nafasi zao, mahali ambapo ataweza kuwabariki na kumweka miongoni mwao Mmoja ambaye Yeye aliahidi Angelimweka miongoni mwao. Iliwapasa wawe katika nchi yao. Kumbukeni, iliwabidi watoke katika ile nchi walikokuwa na waingie katika nchi ya ahadi, kabla Masihi wao aliyeahidiwa hajaja.

44 Na inabidi Kanisa lifanye kitu kile kile. Watoke kwenye lile kundi la wakanaji na kwenda kwenye Ahadi, kabla Masihi hajadhihirishwa mbele yao. Mnaliona hilo?

Uzima wa Masihi uliodhihirishwa kuliandaa Kanisa, Bibi Mwanamke huolewa na mwanamume na kutopatana naye, itakuwa namna ya fujo siku zote. Lakini mume na mke wake, mpenzi wake, huyo aliyemposa, wanapokuwa katika amani kamilifu, kama nafsi moja na nia moja, kwa sababu wanakwenda kuwa mwili mmoja. Basi Kanisa linapokuwa katika amani kama hiyo na Mungu hadi udhihirisho wa Bwana Arusi unadhihirishwa katika Bibi Arusi, kwa sababu wanakwenda kuwa Mmoja. Ama, ni somo kuu mno. Vema.

Vema, sasa kumbukeni, akili za kiroho zikichukua hili zinaweza kuona mfano na kinyume cha mfano na kuchukua moja. Tungeweza kuendelea kwa masaa juu yake. Tazama kile kinachotokea..

45 Na, kwa nini tumesubiri miaka yote hii tangu huu wakati wa furaha kuja?

Mnajua, Biblia hunena kuwa Kanisa lilikimbilia jangwani, lilikolishwa kwa nyakati na wakati. Na kwa nini haya yote yamekuwa? Kwamba sisi... Mnaona, bado ni gurudumu la Mungu ndani ya gurudumu. Kwa nini Mungu hajafanya hili muda mrefu uliopita binadamu alipokaa chini na kalamu za risasi-na wanawake-na kujaribu kuchora wakati kama, Jaji Rutherford na wengine wengi, na Yesu akaja miaka kumi na nne, na mama Shipton na kule nyuma kupita hilo na kadhalika-nyakati hizi zote na ... unaona, walipokwenda kwa kile walichojaribu kuwazia Andiko, unaona, waliharibu.

Limefichwa, kweli limefichwa. Na jinsi gani Andiko litakuwa kinyume Chake Lenyewe wakati Yesu alisema, "Hakuna mtu ajuaye dakika wala saa." Unaona, wanachukua tu kipande kimoja cha Andiko na kukishikilia.

46 Lazima uchukue jambo lote. Basi kama Mungu yupo ndani ya hilo, basi Mungu atadhihirisha hilo kuwa Kweli. Kama uponyaji wa Kiungu, kama sio Kweli, basi sio Kweli. Mungu hatakuwa na lolote la kufanya nao, Iakini kama Yeye anaudhihirisha kuwa Kweli, basi ni ile Kweli.

Kama tu Yesu…

47 Mungu alisema "Kama kuna yeyote miongoni mwenu, nabii au wa kiroho, nitanena naye. Na kile yeye anachosema kikitukia basi kisikieni." Hilo ndilo lenyewe. Lakini kama unabii wake ni wa uongo, basi Mungu hawezi kuwa mwongo. Yeye hana mwisho, hakosei, mwenye enzi yote, na Yeye hawezi kukosea. Kwa hiyo, kama mtu ananena, basi inaonyesha yule mtu-kama alinena maneno yake mwenyewe, yatashindwa, lakini kama akinena Maneno ya Mungu, hayawezi kushindwa, kwa sababu ni Mungu ananena. Ndipo uvuvio wake huja kutoka kwa Mungu, na inapasa liwe sahihi. Hivyo ndivyo Mungu alivyosema lisemwe.

Hivyo ndivyo Biblia... Katika Agano la Kale, Yeye alisema, "Kama wakinena kinyume na torati na manabii, ni kwa sababu hawana Uzima ndani yao," hakuna Uzima ndani

yao, hiyo ni sahihi. Inabidi wanene kufuatana na torati na manabii. Na kama manabii, au kitu kingine chochote lazima kiwe sawasawa na Neno, kama sivyo, ni kosa. Unaona?

48 Sasa, tunakuta kwamba hili lote limetokea kwa sababu... lilisubiri... miamsho-Wamethodisti, Walutheri, Wababtisti, Wakempubeli, na wote hao; wamekuwa na miamsho. Wanazareti, Pilgrim Holliness, na Wapentekoste, wote wamekuwa na miamsho mikuu; lakini kule kutoka kuliko kukuuu hakujaja. Kwa nini?

Mungu alimwambia Abrahamu Yeye angemweka katika ile nchi wakati ule ule, lakini chukizo la Waamori lilikuwa halijatimia. Na Mungu amengojea kwa saburi. Wale watu waki jaribu kuwazia; wanaweza kuona Andiko likiingia katika jambo fulani moja kwa moja-likiingia moja kwa moja katika jambo fulani na kusema, "Hii ndiyo ile siku; huu ndio ule wakati," Iakini mnashindwa kuelewa kuwa chukizo la Waamori halijatimizwa bado.

49 Miaka mia nne, wangesafiri kule Misri na kutolewa nje; lakini kwa kweli walikaa miaka 440, kwa sababu ya kumkataa nabii. Iliwabidi wateseke miaka-mingine kama arobaini kule jangwani kabla Mungu hajawatoa nje. Musa alikuwa kule jangwani miaka arobaini kabla yeye hajarudi kuwakomboa, unaona. Miaka arobaini ya ziada ilipita, ilipita, kwa sababu waliukataa ujumbe.

Sasa, miaka arobaini katika muda wa Mungu ingekuwa kwenye dakika moja na nusu katika muda wetu. Hiyo ndiyo rofauti iliyoko, miaka elfu moja ni siku moja tu, unaona, ni vigumu hata kutimiza dakika moja. Tazama katika hilo.

50 Sasa, tunachelewa. Kwa nini? Mungu amekuwa mvumilivu, akisubiri, akitazama. Akaiachia Lutheran ikainuka katika uamsho-ndipo ikaunda shrika Ia dini. Akawaachia Methodisti iinuke katika uamsho-ikaunda shirika la dini. Akamwacha John Smith wa kanisa la Babtisti ainuke na uamsho mkuu-akaunda shirika la dini. Akawaacha Wapentekoste wainuke na kurejeshwa kwa karama-wakaunda shirika la dini: hadi chukizo lijae kabisa, ndipo Mungu anakuwa amechoka.

Ndipo kutoka kukaja.

51 Na tunakuona kutoka; kwamba watu wenyewe wanaweza kuona kule nyuma ule mtiririko wa wakati, kwamba lile jambo limelaaniwa. Wanachukua kabari na vazi zuri la Kibabeli. Na hilo ndilo jambo ambalo hulaani miongoni mwa watu, mtu anapojaribu kuingiza mawazo yake mwenyewe kuhusu mambo.

lnatubidi tukae na lile Neno-kwamba amri za Mungu hazikuwa na kugusa chochote katika ule mji, ule mji uliolaaniwa. Usiuguse, yaache.

Na Akani alifikiri kuwa angechukua hii kabari ya dhahabu na kuishi kwa anasa sana kama ulimwengu... na vazi zuri la Kibabeli. Ee, kwenye kambi za Waakani, unaona. Lakini lile jambo limelaaniwa, na linaendelea kulaaniwa. Lililaaniwa tangu pale kwenye Baraza la Nikea kule Nikea, Rumi. Limelaaniwa tangu hapo, lakini Mungu ameachia uovu ujae hadi wakati wa Waamori utimizwe.

52 Na sasa, yeyote mwenye ufahamu wa *kiroho*, kumbuka, naendelea kunukuu, "ufahamu wa kiroho." Unaweza kuona kuwa uovu wa taifa hili umekithiri. Limeunda shirika la dini na kurudia kuunda shirika la dini, na kuunda shirika la dini na sasa limekuwa shirikisho na kujiunga na kitu kingine. Uovu umekithiri. Ni wakati wa kutoka.

Ni wakati wa kuitwa nje kwenda Nchi ya Ahadi. Siyo ahadi ya kwenda tu nchi nyingine bali nyumbani, Utawala wa Miaka Elfu Moja-wakati wa kuitwa nje-uovu wa taifa hili ... nitaligonga hilo tena usiku huu, Bwana akipenda… umekithiri! Taifa hili ni chafu!

Unasema, "Ndugu Branham, lile taifa unaloishi ndani yake?" Ndiyo, bwana! Hakika! Unasema, "Ukiwa raia wa Marekani, hungepaswa kusema hilo."

Basi Eliya hangepaswa kuleta laana juu ya Israeli, na yeye akiwa Mwisraeli basi! Wale manabii wengine kamwe wasingelaani lile taifa, hali wao walikuwa Waisraeli.

53 Lakini, walinena tu, siyo mawazo yao wenyewe, ila Neno la Bwana. Inategemea pale unakotoa uvuvio wako; inategemeajinsi gani linakuja na kama liko kinyume na Neno, liache. Na namkaribisha kila mtu yeyote: kuthibitisha kuwa hilo ni kinyume na Neno.

Je, Biblia haikusema katika Ufunuo 13 ... (hapo ndipo hili taifa linakoonekana.) Hili taifa limepewa tarakimu ya kumi na tatu, taifa la mwanamke. Ni mwanamke katika

Biblia. Mwanamke yuko kwenye sarafu zetu. Ni taifa la mwanamke.

Hapo ndipo uozo wa wanawake unapoanzia, unaanzia, ndiko ambako unaishia. Uozo ulianzia katika Edeni kwa kutoliamini Neno la Mungu. Hapa ndiko ulikoanguliwa, wahubiri wanawake na kila kitu kingine. Uchafu wa ulimwengu unatoka kule Hollywood, taifa baya kuliko yote ulimwenguni. Talaka nyingi kuliko za sehemu zote za ulimwengu zilizobakia zikiwekwa pamoja, unaona.

Kwa nini? Utagundua katika mojawapo ya siku hizi, Bwana akipenda. Utaona kwa nini hili jambo lililolaani wa ... U naweza kuona upofu wa hiki kitu cha talaka ambacho Shetani ameweka kwenye macho ya watu. Tuko kwenye wakati wa hatari. Ule mwisho umekaribia kabisa, sasa, naamini. Wameoza, wameoza hadi kwenye kiini.

54 Taifa hili linatokea katika Ufunuo 13, tarakimu ya kumi natatu. Na kumbuka, liliinuka kama mwanakondoo. Uhuru wa dini, lakini basi, lilipata uwezo kutoka kwa mnyama, alama kama hiyo. Na yeye alinena kwa mamlaka yote na kufanya mambo yale yale yaliyooza aliyofanya yule mnyama kabla yake. Basi niambie kuwa halikutabiriwa juu ya hili taifa.

Ile hali ya Kiamori iko karibu kukomaa, kwa sababu tayari wanatenda kazi ndani yake! Na hata papa wetu mpya, kusudi lake kuu ni kuwaunganisha ndugu pamoja! Na kwa macho ya kawaida, ndilo jambo la kufanya! Lakini katika macho ya Mungu, ni kinyume na Roho Mtakatifu! Hatuwezi kuchanganyika na hilo. Na kila kanisa litanaswa katika shirikisho hilo!

Toka nje ya hicho kitu haraka uwezavyo! Nawe utachukua alama ya mnyama, bila kujua kile unachofanya! Toka ndani yake!

55 Natumaini akili za kiroho zinaweza kulidaka hilo, nina hakika mnalidaka, lakini sijui kuhusu nje kule. Vyovyote vile, huwezi kutembelea kila taifa, unaweza kutuma kanda kila nchi. Mungu atakuwa na njia fulani ya kupata ile nia kule ambako ile mbegu imepandwa. Hiyo ni sahihi. Na mara tu Nuru inapoigonga, imekwenda, inapokea Uzima! Kama yule mwanamke pale kisimani, alisema, "Hilo ndilo jambo lenyewe," alilipata.

Toka kwenye hicho kitu, kimelaaniwa. Kimelaaniwa, niambie ni wapi yeyote aliwahi kuanguka na kuinuka tena. Niambie mmoja aliyewahi kuinuka ambaye hakuanguka. Kwa hiyo, unaweza kuona kuwa kile kitu ni kosa.

56 Vema. Uovu wa Waamori ulikuwa bado haujajaa hivyo inawabidi wakawie na kusubiri kabla ya kule kutoka. Lakini uovu wa Waamori unapojaa, basi kunakuja kutoka kwa kiroho au kutoka kwa kawaida, kuwaongoza watu kwenda nchi ya asili, pale ambapo Mwamori wa asili alikowahi kukaa wakati mmoja-waliita hiyo nchi yao.

Na uovu wa dhehebu la Mwamori, wale waliojiita wenyewe kanisa kwa muda mrefu, hadi uovu wao unakaribia kutimizwa. Kutoka kunakuja ambako Mungu ataonyesha nani ni nani, pale ambapo Kanisa lenyewe, Bibi Arusi wa Yesu Kristo atakuwa "ametolewa" nje kwenda katika nchi iliyoahidiwa-katika Nyumba ya Baba Yangu kuna makao mengi katika hapo mahali.

Hatuhitaji kwenda kule na kupigana kama walivyofanya, imetayarishwa tayari. Kama hii nyumba ya maskani ya duniani ikiharibiwa, tunalo jengo litokalo kwa Mungu ambalo tayari linatungojea. "IIi pale Mimi nilipo, ninyi nanyi muwepo pia." Kutoka kukuu kunakokaribia.

57 Tazama jinsi Mungu alivyofanya kutoka kule. Kile Yeye... yale matayarisho Yeye aliyofanya, na uzingatie kwa dakika moja, ndipo utazame yale ya leo.

Vema, tazama, kabla ya kutoka huku, aliinuka farao ambaye hakumjua Yusufu, unaona, farao ambaye hakumjua Yusufu-hakumjua Yusufu. Yusufu alikuwa anamwakilisha nani, sehemu ya kiroho katika kutoka huku kwa kiroho. Sasa pale kunainuka-asemaye tuko huru.

Yule mwanamke alilishwa kwa wakati, wakati na nusu ya wakati.

Lakini mwishowe aliinuka ... farao, kiongozi wa kidikteta, ambaye hakujua uhuru wa dini. Akiwaunganisha wote. Usiliache hili likupite. Utakuja wakati ambapo kulikuwa na farao, kwanza, ilibidi atokee. Na mashirika ya dini yameishi kwa utamu sana, yameishi kama tawi lililopandikizwa kwenye mti usio wake katika mzabibu halisi wa Ukristo, lakini bado likizaa matunda yake ya asili.

Wanawake wamevaa nusu uchi, wanaume wameelimika na kukataa nguvu za Roho, lakini yameishi chini ya jina la kanisa la Kikristo. Ni tawi la mzabibu IiIilopandikizwa kwenye mti usio wake, lakini mkulima anakuja sasa kupunguza matawi ule mzabibu, kama Yeye aliovyosema Yeye angefanya. Na yote yale yasiyo na matunda yangekatiliwa mbali na kutupwa katika moto na kuteketezwa.

58 Ni jambo la kutisha kusema, lakini KweIi wakati mwingine huonekana ya kutisha. Inakuambia tu- jinsi Mungu anavyochukua watoto Wake kupitia maji yenye kina kirefu na mchanga wa matope na mambo kama hayo. Yeye hulifanya hilo kwa njia hiyo.

Kumbuka, chungu lazima kivunjwe vipande vipande. vitu vilivyofungwa pamoja, vipande vidogo, kifinyangwe na kusagwa tena. Inaonekana kama jambo la kutisha kukivunja, lakini inabidi lifanyike hivyo, ili kwamba kuunda kile chungu tena, jagi la kuwekea maua au chochote kile unachotengeneza.

59 Kulikuwa na farao aliyeinuka. ambaye hakumjua Yusufu, na huo ulikuwa mwanzo wa ule mwanzo. Huo ulikuwa ndio mwanzo wa kutoka. Na hilo jambo Iilipoanza kujiunda chini ya nguvu ya kisiasa, lilianza kujiunda. Mungu akaanza kujitayarisha.

Uovu wa Waamori ulitimia. Wakati ule Yeye aliomwahidi Abrahamu ulitimia, na wakati wa ukombozi ulikuwa umekaribia. Na Mungu aliruhusu farao ainuke ambaye hakumjua Yusufu, na Raamses alizaliwa. Mara tu baada ya Seti anakuja Raamses, na Raamses alikuwa yule asiyejua baraka za Yusufu.

Yeye hakujua upande wa kiroho uliko, yeye alikuwa-mtu mwenye akili ya kisiasa tu, kwamba angeweza kukamata Ethiopia na nchi nyingine zote chini ya uwezo wa kijeshi, na hilo ndilo tu yeye alilojua lilikuwa uwezo wa kijeshi.

60 Na nafikiri kama mtu yeyote ni wa kiroho, angeweza kuona kile kinachotokea sasa. Tunampata farao asiyejua uhuru wa dini. Rais wetu alipoingia madarakani, hakuapa kwa hilo, kwamba aliamini katika uhuru wa dini.

61 Vipi kuhusu siku ile nyingine tulipokuwa na hili swala la ubaguzi, chini kule kusini? Wakati huyu gavana wa Alabama... Natamani ningezungumza na yule mjumbe wa serikali-yule... Martin Luther King, jinsi gani mtu angekuwa kiongozi na kuongoza watu wake kwenye mtego wa kifo?

Kama wale watu wangekuwa watumwa, ningekuwa chini kule, nikiwa nimevua koti langu, nikiwapigania wale watu. Wao sio watumwa, wao ni raia; wao ni raia wa taifa.

Swala la kwenda shule... Wale watu-kama wana moyo mgumu na hawajui hayo mambo, huwezi kuingiza ndani ya watu mambo ya kiroho, kile kilichogongewa pale kwa nguvu za kisiasa. Inawapasa walikubali, wazaliwe upya, na ndipo wataona haya mambo.

62 Lakini huyu mtu, kama ningeweza tu kuzungumza naye-akiongoza wale watu wa thamani, kwenye mtego wa kifo chini ya jina la dini, ambapo anakwenda kuua maelfu mara maelfu yao. Wao hawa ... wanaelewa tu upande wa kawaida.

Huyu mtu ... ndugu ambaye ni mweusi-yale maasi makubwa yalipokuja Louisiana, nilikuwa kule wakati ule. Wakati... kuna mhubiri mmoja chotara, ndugu mzee wa thamani, alisimama kule na kusema, akawaomba wanamgambo, "Je, ninaweza kuzungumza nao; ni watu wangu."

Na huyu mtumishi mzee akasimama kule na akasema, "Nataka kusema asubuhi hii, sikuwahi kamwe kuonea haya rangi yangu. Muumba wangu aliniumba kile nilicho."

Hivyo ndivyo Yeye anataka ubakie. Hivyo ndivyo Yeye anataka kila mtu abakie. Yeye huumba maua meupe na maua ya bluu na rangi zote za maua. Usichanganye mbegu zao. Usiyachanganye. Unakwenda kinyume na asili.

63 Akasema, "Kamwe sikuwahi kuonea aibu rangi yangu, hadi asubuhihii." Akasema... Ninapoona watu wangu wakiinuka na kufanya mambo wanayofanya sasa," akasema, " inanifanya nione aibu juu yao."

Nikawaza, "Mungu ambariki yule mtu."

Akasema, "Mnakwenda tu kusababisha shida." Akasema, "Angalieni mashule hapa. Kama tusingekuwa na mashule, akasema, "ingekua tofauti, lakini nani wenye shule nzuri zaidi hapa, katika Louisiana?"

Akasema, "Hebu kwa mfano tuchukue mji wetu, Shreveport." Akasema, "Kuna shule ya weupe kule ambayo ni shule ya zamani. Wamejenga nyingine. Hawana hata

kifaa kimoja, hata kitu kimoja cha watoto cha kuchezea, sisi tunavyo vimejaa kiwanjani. Na zaidi ya hilo, wametujengea bwawa kubwa la kuogelea la marimari kwa ajili ya watoto: na tunao walimu wazuri zaidi ya wote wanaoweza kupatikana.

Akasema, "Kwa nini mnataka kwenda kule, hali tunacho kilicho kizuri zaidi hapa? Mna tatizo gani?" akasema.

Na wale watu wakasema a-a-a-ah na wakapunguza sauti. Hivyo ndivyo. Unaona?- uvuvio wa makosa.

64 Wale watu walikuwa watumwa. Wao ni ndugu na dada zangu. Kama wangekuwa watumwa, ningesema, "Hebu tuungane nao na kwenda kuandamana barabarani na kupinga lile jambo."

Wao sio watumwa. Wao ni raia wenye haki zote ambazo yeyote mwingine anazo. Ni kundi tu la msukumo wa roho linalotoka kuzimu kusababisha milioni kati yao wauawe. Wataanzisha rnapinduzi, hakika ni hivyo. Siyo sahihi.

Wanaume na wanawake wana haki zao wenyewe. Ndugu zetu weusi na Wajapani wetu na wale wa njano, weupe na weusi na vyovyote walivyo-hakuna tofauti katika rangi ya Mungu wetu. Sote tunatoka kwa mtu mmoja, Adamu. Lakini kama Mungu alitutenganisha na kutufanya rangi tofauti, hebu tubakie hivyo. Kama ningekuwa mtu wa njano, ningependa nibakie Mjapani au Mchina. Kama nilikuwa mweusi, nigependa kubakia hivyo, Mungu aliniumba hivyo.

65 Kwa kweli kuna mengi kuhusu jamii ya weusi ambayo jamii ya wazungu inapaswa iwe nayo. Wao hawana woga, wao ni wa kiroho zaidi. Kuna mambo elfu kuhusu wao ambao mzungu hata hawezi kugusa. Mungu aliwaumba hivyo. Nani ataweza kuimba Vizuri kuliko kwaya ya watu weusi? Utapata wapi sauti hizo?

Nimeona wakija toka nchi za huko mbali, hawakujua kilicho cha mkono wa kuume wala wa kushoto. Makabila thelathini au arobaini yaliyo tofauti, na wanaimba hadi mahali walimu wanasimama pale na kusema, "Siwezi tu kufikia kiwango hicho."

Hawa wana kwaya zilizopewa mafunzo miaka na miaka na nyingine zitakuwa na ufundi wa kuimba kwa kupandisha tuni juu hadi ya nane na kushusha chilni ya kila kitu, nao watasema, "Hebu sikiliza hiyo," kamilifu tu, hata katika lugha tofauti. Wao wana kipaji.

66 Lakini unaona, haya mambo yote inabidi yatokee; yote kwa sababu ya mwanasiasa yule ninyi watu mliomchagua kwa mashine zenu za upotofu. Juzi juzi, yule gavana aliposimama pale, akaapishwa na kuchaguliwa katika iIe ofisi, na watu, na swala la ubaguzi kufuatana na katiba ilivyo, kwamba kila jimbo linaweza kuwa na wazo lake lenyewe kuhusu hilo.

Yeye hakujali, lakini alisoma katiba na kusema, "Sasa, shule yetu inaunga mkono ubaguzi wa rangi. " Wanayo shule juu kule, na ni watoto wawili tu weusi waliotaka kuingia ile shule wakati wanacho chuo chao wenyewe. Lakini alisimama na kusema... Kile alichofanya... yeye alisoma ile katiba.

67 Basi linaporudi kwa huyu mtu tuliye naye hapa ambaye hamjui Yusufu, uhuru, akichuma zile kura za watu weusi, na bila kujua kwamba, kwanza, kilikuwa chama cha Republican kilichowaweka huru, wakiuza haki zao za kuzaliwa kwa kitu kama hiki kiwaongoze katika mtego wa kifo kuonyesha kuwa kila mfumo ulioundwa na mwanadamu lazima ushindwe. Hiyo ni sahihi kabisa.

Na bwana Kennedy, alililifanya lile jambo kuwa tatizo la kitaifa na akawatuma "askari" kuwarudisha wale watu moja kwa moja katika nyuso za baba zao wenyewe, wakisimama pale chini ya katiba ile iliyovunja katiba tena.

68 Akasema,. "Hatutapigana, hapana, bwana," na kusema, "Natumaini taifa linaweza kuona kuwa hatuishi tena chini ya demokrasia, ila chini ya udikteta wa kijeshi."

69 Mnajua ule msemo wa zamani, "Ukishawahi kuwa M-Democrat wa kusini, basi utaendelea kuwa hivyo siku zote." Sijui sasa. Hakika mtu atakuwa na busara ya kutosha kuzinduka kuona jambo fulani. Waacheni wale watu wa thamani, msiwaue chini kule. Kama yule mtu, aliyempiga risasi yule ndugu mgongoni usiku wa juzi kwa ile bunduki, watoto wake wachanga na mke wake ndani ya nyumba. Sijali yeye ni nani, hilo ni jambo la kishenzi na la ovyo. Naam, bwana.

Ningependa kuwa hakimu juu ya hiyo kesi siku moja. Kumpiga risasi yule mtu akija nyumbani kwa mke-wake na watoto-yeye ni raia, anayo haki kusimamia kile anachowaza kuwa ni sahihi, mtu mzuri.

Ile picha katika gazeti la Life-yule mvulana mdogo akimlilia baba yake; na haini mmoja nje kule, akampiga risasi mgongoni kutokea mafichoni. Huko ndiko unakokwenda unapomkataa Kristo. Hiyo ni sahihi, Hapo ndipo taifa lote limefika, yote chini ya siasa. Ni aibu hivyo, lakini, hilo ndilo tulilotaka. Tulithibitisha katika huu uchaguzi.

70 Mwanangu mdogo alisema nami asubuhi hii, "Baba, je, wale Waingereza waliohamia Marekani na kuanzisha makoloni huko yaliyokuwa na uhuru wa kidini, walipokuja hapa, je wote walikuwa wa hili kanisa la dhehebu fulani? Je wote walikuwa…" akasema, "Walikuwa wamevaa makoti makubwa."

Na nikasema, "Hapana, mpenzi, walikuja hapa kwa ajili ya kupata uhuru wa kidini. Hilo ndilo walilojia hapa ni kuondokana na kuwa chini ya kitu kama kile."

Unaona pale yalipofikia sasa? lnaonekana kuwa falme zote hizi lazima zianguke. Lazima niharakishe.

71 Jambo moja ninaloomba ni yule Ndugu Martin Luther King aamke kikwelikweli mapema. Yeye anawapenda watu wake; bila shaka. Lakini kama tu yeye-ataona pale msukumo wake...

Utafaidi nini kama utakwenda shule na milioni moja kati yenu wamelala pale wamekufa? Si ingekuwa tu sawa kutokwenda shuleni?

Sasa, kama ni kwa ajili ya njaa, kama ilikuwa kwa ajili ya kitu kingine-watumwa, yule mtu angekuwa mfia dini kutoa uhai wake kwa njia kama hii, njia nzuri; na hiyo ingekuwa njia inayostahili. Lakini kwenda tu shule, silioni hilo.

Sidhani Roho Mtakatifu anakubaliana naye hata kidogo juu ya hilo. limefanya hao watu wawe wanafanya fujo na kupiga makelele, unaona. Kama tu Hitler alivyofanya kule katika Ujerumani, aliwaongoza moja kwa moja katika mtego wa kifo, wale Wajerumani wa thamani; nao wakalala kwa mabilioni, au mamilioni, wamelundikwa kule mmoja juu ya mwingine. Hilo ndilo jambo lile lile hasa, na kumbuka niko kwenye kanda, utaona hilo labda baada ya mimi kuondoka.

Hilo ndilo hasa linalokwenda kutokea. Wale watu wa thamani watakufa chini kule kama nzi. Wanaanzisha mapinduzi, wote weupe na weusi watapigana tena na kufa kama nzi. Na mtakuwa mmepata nini wakati mambo yatakapokuwa yamekwisha?- kundi la watu waliokufa.

72 Lakini kuliinuka farao ambaye hakumjua Yusufu. Ni jambo lile lile leo. Mtu ameinuka na kula kiapo katika Ikulu ambaye hataapa kwa kiapo chake-hataapa, kwamba anaamini katika uhuru wa dini.

Huyu papa mpya anasemaje? Moja-anayo mambo manne. Mojawapo ni kuwaunganisha Waprotestanti na Wakatoliki pamoja. Na kwa mtu yeyote mwenye akili, hilo ndilo jambo la kufanya, Lakini kulingana na Biblia, ni jambo la-makosa kufanya, na Biblia ilisema, wangelifanya hilo. Hebu tuendelee mbele kidogo.

Kwenye wakati huu Ramisesi katika Misri alikuwa anakua. Uwezo wake unaongezeka. Mtu wa kawaida, Ramisesi, alikuwa anakua. Mtu wa kawaida, mpingaKristo, anakua sasa kupitia siasa. Yeye ameshaingia lkulu tayari.

Katika dini, yeye amewafanya watu kuwa na mawazo yaliyovurugika yasiyokuwa na msingi ambayo kwa hakika wataanguka moja kwa moja kwa ajili ya hilo. Na viongozi wa madhehebu... kwa kweli kila kanisa lililopo katika taifa tayari lipo katika shirikisho la makanisa. Ramisesi anakua, na wote wataungana pamoja, na hilo ndilo watakuwa nalo. Nalo linafanya nini? Linaunda nguvu, mnyama kama yule wa kwanza.

73 Ndipo kunakuwa na mateso yanakuja juu ya wote wale ambao hawataungana nalo, na kugoma. Utakuwa umechelewa kupita kiasi, tayari umechukua alama. Usiseme, "Nitalifanya hilo baadaye;" ni bora ulifanye sasa. Ramisesi alikuwa anakua.

Lakini, kumbuka Ramisesi alipokuwa anakua katika nguvu za Misri, Mungu alikuwa na Musa kule jangwani. Yeye alikuwa anakua pia. Ramisesi alikuwa na mfumo wa siasa. Mungu alikuwa na mfumo wa kiroho chini ya nabii aliyekuwa tayari kuja-chini na kusema

na watu.

74 Wote wanakua tena. Itakuwa ni onyesho la mwisho la makusudio mojawapo ya siku hizi. Wakati haupo mbali na pale ambapo kutakuja onyesho la mwisho la makusudio.

Kama ile asili-kama Andiko linavyosema, "Ile ya asili ni mfano wa ile ya kiroho". Huwezi kulikwepa hilo. Lipo hapo, liko moja kwa moja mbele ya macho yako. Ni Ukweli.

Tazama Kanisa sasa, likiita, likija katika uwezo. Roho Mtakatifu akishuka. Mafumbo ya Mungu yakifunuliwa na kuwekwa katika utaratibu, unaona. Kanisa halisi-liko lkulu tayari, na Kanisa linajikusanya pamoja-sio dhehebu, lakini mbali na kifungo cha maovu, mbali na Waamori. Watu walio huru. Loo!

75 Mungu alikuwa na Musa, nabii Wake mtarajiwa, ingawa alikuwa tayari ameshatabiri, na alikuwa amethibitisha kuwa yeye alikuwa sahihi, lakini bado, yeye alikuwa katika shule ya jangwani, amefichwa mbali na ulimwengu. Lakini yeye alikwenda shule, akiwa anafundishwa, nje katika jangwa.

Adui siku zote atapendekeza, mfumo wake na kutokuamini kutalipokea, kwa sababu adui ni ishara ya kuenenda kiakili. Sasa, kumbuka, kuna mbili tu ... Usilisahau hili. Kuna nguvu mbili tu. Moja ni nguvu ya kiroho ya Roho Mtakatifu, ile nyingine ni lbilisi akitenda kupitia nguvu ya akili. Kwa pale ndipo yeye alipoingilia katika Bustani ya Edeni-kupitia nguvu za akili, kumfanya Hawa aamini katika dhana ya kiakili dhidi ya Neno. Liko wazi tu kama liwezavyo kuwa, watoto wachanga wangeweza kulipata hiIo, unaona. Na hiyo ndiyo njia iliyokuwepo kote kurudi nyuma.

76 Liko hana katika Misri asubuhi hii.

Kuna nguvu ya akili inayotenda kazi ya Ramisesi, ikimleta kwenye nguvu na kumwinua, ambaye hajui uhuru-kile Yusufu alichofanya, kile Kanisa lilichofanya hapo mwanzo.

Na sasa, tunaona jambo lile lile, nguvu ya kiakili ikijiingiza miongoni mwa makanisa, na imeinua mkuu wa kanisa, ambaye hajali kuhusu kile Biblia inachosema. Wanao mfumo wao wenyewe, sio kile inachosema Biblia; ni kile kanisa linachosema.

Na Waprotestanti waliingia moja kwa moja ndani ya hilo hadi makundi yote kama hili ... "Vema, hakika, najua linasema *hivi*, lakini nawaambia, zile siku zimepita." Mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu. Kila Andiko katika Biblia linaelekeza moja kwa moja kwenye hilo.

Sasa, unaona ni kwanini nilitaka kurekodi hili, na kulituma kwa watu. Ile saa imefika! Inabidi Kweli ijulikane! Kutoka kumekaribia! Unaona? Ile sehemu ya kiakili inaonekana kamilifu, na ni kamilifu. Ni hasa ... lakini kamilifu, uvuvio wa Shetani.

77 Na ndipo wakati wote ambao huyu Ramisesi mwerevu alipokuwa anakua na kuja kwenye kiti cha enzi... Na kumbuka, alikua akiwa kama kaka yake Musa, unaona, kaka yake Musa. Mmoja wao ilibidi achukue kiti cha werevu, kama tu Yusufu kwa ndugu zake. Na walifanya nini na Yusufu mdogo?-walimtenga kutoka kwenye neno. Neno ni Mungu. Na wao walilitenga Neno na kupokea kanuni ya imani, na sasa, kanuni ya imani imekua na kuwa uwezo. Ee, Mungu, hebu watu waone hilo!

Jinsi gani nitatumia sauti zaidi? Jinsi gani nitalifanya wazi kwa Maandiko chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, kwamba tuko hapa? "Loo," unasema, "vema, sasa, kama hilo lingekuwa limekuja toka kwa Papa Yohana, au Papa Fulani, au Askofu Fulani…

Unaona kuwa Mungu alimchukua mkaaji wa jangwani aliye duni? Unasema, "Jinsi gani hilo Iote Iaweza kuwa makosa?"

78 Mungu hushughulika na watu binafsi, sio na kundi, na watu binafsi. Mungu anampa yeye... anapata... kitu pekee Yeye alichokuwa nacho ni mtu mmoja ambaye Yeye angefanya kazi naye. Hilo ndilo lote Yeye analotaka, ni mtu mmoja.

Yeye amejaribu kuwa nalo kupitia kila kipindi, kama Yeye angeweza kupata mtu mmoja. Yeye alipata mtu mmoja katika siku za Nuhu; mtu mmoja katika siku za Eliya; mtu mmoja katika siku za Yohana Mbatizaji. Yeye anataka mtu mmoja tu.

Katika siku za Waamuzi, Yeye alijaribu kumpata mtu mmoja, Samsoni. Akampa nguvu kuu, lakini yeye aliiuza kwa mwanamke na akapofushwa. Waamuzi, haikuwa hivyo, Mungu ni Mwamuzi, unaona.

Unaona leo, Yeye anajaribu kumpata mtu mmoja, Yeye anaweza kupata mkono

Wake... ambaye unaweza kusema ile Kweli, ambaye hautakuwa na woga na hilo; ambaye hatakubali kupunguza nguvu ya mashambulizi, ambaye hatakuwa na kanuni. Mtu mmoja ambaye Yeye anaweza kumshikilia katika mkono Wake na kuonyesha Neno Lake lililo hai na kujionyesha Yeye Mwenyewe kuwa Hai.

Naamini Yeye anaweza, kupata mtu kama huyu akiwa tayari. Naamini, naamini hilo, naamini tu Biblia vya kutosha kuliamini hilo. Yeye angeweza kumpata, hilo ni sahihi, ambaye ungesema Ukweli.

79 Baada ya muda kidogo tunakuta, baada ya kupitia hizi shule zote... Sasa tazama, adui anapendekeza jambo fulani-akili ya werevu, kwa sababu adui anafanya kazi juu ya akili. Na akili itatulia na kulifikiria na kusema, "Sasa, subiri kidogo. Je, sio kwamba baraza ... " Nilizungumza na mtu siku ile nyingine, naye akasema, "Tazama, Billy ... " (Yeye anafanya kazi kwenye Kampuni ya Huduma ya Jamii, mtu mzuri.) Na yeye akasema, "Nataka nikuulize jambo fulani." Akasema, "Wewe ni M-Irish."

Nikasema, "Ndiyo, bwana," nikasema, "Kwa namna fulani nalionea aibu, lakini bado, ndivyo nilivyo."

Na yeye akasema ... "Vema," akasema, "hujui kwamba wewe, kwa kweli ungekuwa Mkatoliki. "

Nikasema, "Mimi ni, Mkatoliki wa asili."

Unajua, kanisa la kwanza lilikuwa kanisa Katoliki. Unaona pale lilipofika leo? Lilianza pale Pentekoste, lakini shirika la dini limeliweka pale lilipo leo. Tazama Pentekoste, limerudi nyuma moja kwa moja na kufanya shirika la dini, na kufanya mambo kanisa la kwanza la Katoliki-na karibu sana kuwa mbali leo kama walivyokuwa katika miaka 2000, na miaka hamsini imewaleta karibu sana nalo. Mnaona?

80 Yeye akasema, "Je, huamini, kwamba wakati kundi la mwungano wa makanisa (hilo ndilo lenyewe) litakapokaa pamoja na kuwaza jambo, na kundi lote liweze kukubaliana, je hudhani wangekuwa tu kidogo... " kusema, "Huwa nakuja kusikiliza ukihubiri," akasema, "lakini sikubaliani na wewe."

Na nikasema, "Njia pekee ambayo unaweza kuthibitisha kuwa kutokubaliana kwenu kumejengwa juu ya msingi ulio halisi, ni kulithibitisha kwa Biblia. "

Akasema, "Biblia haina uhusiano na hilo."

Nikasema, "Kwako, inaweza isiwe, lakini kwangu ni yote inahusika nalo," unaona. Ni Neno.

Akasema, "Je hufikirii kuwa kundi la mwuungano wa madhehebu wakiwa wamekaa pamoja wangeweza kuwa sahihi zaidi na kuwa na hakika ya kuwa sahihi kuliko mtu mmoja duni asiyeelimika kama wewe mwenyewe?"

Na nikasema, "Vema ... " Akasema, "Inakuhusu nini hata useme chochote dhidi ya lile-Bi-dhidi ya kanisa letu? Wakati wamekuwepo wakati wote- walipokuwa na baraza la kwanza la kanisa kama ulivyosema juu yake usiku mmoja, tulisikia Vipindi vya Kanisa vya baraza la madhehebu yakikusanyika kule Nikea, Rumi na kuunda Kanisa la Katoliki." Akasema, "Je, hujui kulikuwa watu maelfu, roho, Mungu alituma watu kuketi katika lile baraza? Na je, hudhani kuwa mawazo yao yangeweza zaidi kujua mapenzi ya Mungu, kuliko yenu chini hapa, baada ya Mungu kuthibitisha kupitia miaka 2000 kwamba lile kanisa liko sahihi?"

81 Nikasema, "Yeye hakuwahi kamwe kuthibitisha hilo." Nikasema, "Kama kanisa hilo ni kanisa la Mungu, hebu tulione likizaa matunda kama lile Kanisa la kwanza lilivyozaa wakati ule. Hebu tuone likizalisha mambo yale waliyofanya wakati ule kwanza." Wakati hata Biblia inasema, kwamba hata, "siyo hata lililo dogo au yodi moja katika Biblia haitashindwa kutimia." Na Mungu alisema, "Yeyote atakayeondoa neno moja kutoka katika Hili Neno au kuongeza hapo neno moja, sehemu yake itaondolewa," iwe ni baraza la mwungano wa madhehebu au chochote kile toka kwenye Kitahu cha Uzima, yeye amekwisha.

Akasema. "Billy wewe umepotoka tu."

Na nikasema, "Basi nadhani wakati mmoja, katika wakati mkuu wa heshima katika Israeli, walipotengana kama Protestanti na Katoliki walivyo leo-Israeli ilitaka kubakia Israeli. Lakini nilisema, "Tunakuta kwamba walikuwa na mfalme aliyeitwa Yehoshafati,

mtu wa haki, aliyejaribu kushika amri za Mungu; lakini walikuwa na mwingine hapa aliyeitwa Ahabu, aliyeoa mwanamke, siasa, akijaribu kufanya urafiki na taifa lingine na akaoa mmoja wa mabinti. Yezebeli, na kumleta Yezebeli-miongoni mwa watu wa Mungu-jambo lile lile ambalo tunafanya. Na kuleta ndani... na yeye akawa mtawala. Akamfanya Ahabu aseme *hili* na kumfanya Ahabu aseme *lile*-jambo lile lile mnafanya sasa.‟ Na nikasema, ″Lile dhihirisho la mwisho la makusudio linakuja.‟

82 Walitaka kuunganisha makanisa mawili pamoja kama wanavyojaribu kufanya sasa.‟ Na kwa Ahabu na hata Yehoshafati, mtu wa shirika la dini, akasema, ″Ndiyo, hiyo itakuwa vema.‟ Watu wako ni watu wangu. Sote tu Wakristo. Sote tu waamini. Hebu tuwe pamoja.″

Lakini yeye alipokwenda chini kwenye dhihirisho la mwisho la makusudio, yeye alisema, ‟Hudhani tunapaswa kwenda kwenye maombi kuhusu hili? Tunapaswa kumtaka Bwana shauri.″ Na yeye akasema, ‟Ndiyo.″ Ahabu akasema.

Kwa hiyo yeye akasema, ‟Nitakuambia jambo. Hebu tumtafute nabii wa Bwana.″ Lakini unaona, Ahabu alikuwa na mfumo ambao alifikiri ulikuwa wa Bwana. Akasema, ‟Ninao mia 400, waliosoma na kufundishwa, na wao wanadai kuwa ni manabii wa Kiebrania,″ (kama vikundi vya wahudumu vinavyofanya leo.)

Nao wakawaleta nje na kuwauliza swali kuhusu matokeo ya vita. Na kila mmoja wao wakakusanyika na kuunganika kama tu baraza la mwungano wa madhehebu linavyofanya leo, na wanakuja na swali: ‟Kwea, Bwana yu pamoja nawe, kwani ile nchi hakika ni yetu, na kuwatoa Washami kule, au Wafilisti. Tuwatoe nje kwa sababu ile nchi ni yetu.″ Hilo linaonekana la busara sana. Unaona?

83 Lakini bado ndani ya moyo wa Yehoshafati, halikuonekana sahihi. Yeye akasema, Najua unao pale wahudumu 400 wa mwungano wa madhehebu waliofundishwa vyema, na wao wote wana shauri moja,‟ (Hata wakatengeneza jozi ya pembe na kusema, ″Hivi asema Bwana‟) ″lakini tungeweza tu kupata mmoja mwingine?‟

Akasema, ‟Hebu mfalme asiseme hivyo, ″ alisema yule mwanasiasa. ‟Hebu Mfalme asiseme hivyo, kwa sababu hawa watu ni watu waliopewa mafunzo. Nimewafundisha mimi mwenyewe. Ndivyo hivyo, ndivyo hivyo. ″Nimewafundisha hawa watu, Iakini kuna mmoja zaidi, lakini namchukia.‟ Unaona?

Akasema, ‟Huyo ni Mikaya, mwana wa lmla, lakini akasema, ″Namchukia, Yeye si lolote ila msaliti miongoni mwao. Yeye siku zote anawakaripia wenzake. Yeye siku zote ananiambia kuwa ninakosea, na kutazama ufalme wangu. ‟ Naam, hebu mtazame. Tazama jinsi ulivyokuwa umevurugika.

84 Tazama dhehebu lako leo, likiwa na mfano wa utauwa na kukana nguvu za Mungu. Ee, unaweza ukawa milioni moja zaidi na elfu moja zaidi na mtu uliyefundishwa vyema zaidi, lakini uko wapi katika Roho? Nguvu yako iko wapi kama ile ya Samsoni yeye aliposimarna pale, kama nilivyosema majuzi, akiwa na ule muundo mkubwa wa nyuma. na kila mshipa ndani yake ukiwa mahali pake vizuri, lakini bila Uzima ndani yake.

Roho alimwacha: alikuwa asiyejiweza, mtoto mdogo akimwongoza kote, macho yaliyopofuka, kwa sababu ya mwanamke fulani. Kama kanisa lilivyo leo, limeongozwa kote na siasa, maaskofu, wazee, na kila namna ya vitu. Watu wakijaribu katika hali ya kukata tamaa kupata kitu fulani katika kofia zao na kila kitu. Tuko wapi?

Kwa hiyo, tulifika lini hapa mahali penyewe?

85 Walituma na kumIeta Imla au-siyo Imla, bali Mikaya, mwana wa Imla. Walituma na kumpata yeye, naye akatabiri na akawaambia kuwa Ahabu angeuawa kama akikwea juu kule. Na yule askofu mkuu akampiga kofi mdomoni. Alikuwa mwaminifu kuhusu hilo. Yeye akasema, ‟Roho wa Mungu alikwenda wapi wakati Yeye aliponitoka?″ Akasema, ‟Utaona.″ Uh-huh. Uh-huh. Akasema, ‟Mweke gerezani; mweke jela ya ndani zaidi na alishwe mkate wa huzuni na maji ya huzuni, na nitakaporudi kwa amani,″ akasema, ‟nitashughulika na huyu mtu.″

Na Imla akijua kuwa yeye alikuwa sahihi mbele za Mungu... Kwa nini? Ono lake lililingana na Neno. Yeye alikuwa nabii, na Roho wake na ono lake lilikubaliana kabisa na nabii, Eliya. Akasema, ‟Kama ukirudi kabisa, basi Mungu hakunena na mimi.″

Sasa, nilisema na huyu mtu, ‟Lipi lilikuwa sahihi? Lile baraza la madhehebu pale ambapo watu 400 waliochaguliwa waliketi pamoja, walioteuliwa na mtu, au mwasi

mmoja duni, aliyechaguliwa na Mungu?"

Akasema, "Vema, utajuaje tofauti?"

Nikasema, "Turejee kwenye ramani za majengo. Tunajuaje kujenga jengo isipokuwa kuwe na ramani ya jengo?

Kama wangesita kidogo kwa dakika moja na kukuta kuwa yule nabii, Eliya alimlaani Ahabu. Yeye alisema mbwa wangeramba damu yake, nao walifanya hivyo. Jinsi gani yeye angebariki kile Mungu alichokilaani? Jinsi gani wewe unaweza kubariki chochote kile Mungu alichokilaani?

Toka nje ya kile kitu; kikimbie. Njoo kwa Kristo. Amina.

86 [Sehemu tupu] ...analiandaa hilo, na mawazo ya kiakili husema, "Hilo ni sahihi." Hapo ndipo huyu ndugu wa thamani alikuwa, huyu mtu. Alisema, "Inaonekana kama ... tazama hapa, unajua kwamba kama sisi sote tungekuwa pamoja kama kanisa moja, je hudhani tungekuwa bora kuliko kutawanyika jinsi tulivyo sasa?"

Je hilo halionekani la maana, kama Waprotestanti wote na Wakatoliki wangeungana pamoja na kufikia kwenye maafikiano? Lakini jinsi gani wawili wanaweza kutembea, ila wawe wamepatana? Jinsi gani wewe, wakati kundi moja *hapa* haliamini katika uponyaji, na *lile* lingine linasema wanaamini huo, *lile* lingine linauweka kwenye wakati mwingine huko nyuma, (baadhi yao hata hawaamini Biblia) na kuwaweka pamoja: umekuwa na kitu gani? Mungu sio mwanzilishi wa machafuko.

Kabla Mungu hajaweka Kanisa Lake katika utaratibu, walisubiri siku kumi mchana na usiku hadi wote wakawa mahali pamoja na moyo mmoja, na ndipo akaja Roho Mtakatifu kwa ajili ya uongozi. Siyo Baraza fulani la Umoja wa Madhehebu, unaona? Natumaini mnalipata hili. Tazama.

87 Huyo ni asiyeamini, asiyekuwa mwaminifu kwa Neno la-Mungu ambaye hajali kile Neno lilichosema, lakini anajali fikra zake mwenyewe. Hicho ndicho Hawa alichofanya mara ya kwanza. Alitumainia akili zake.

Shetani alisema, "Sasa tazama hapa, je sio jambo lenye maana hilo? Najua Neno linasema *hivyo*, lakini subiri kwa dakika moja, je sio jambo la maana kwamba ungekuwa bora kama ulijua jema na baya?"

"Mbona, ndiyo ... " Ndipo akalichukua. Hakika. Unaona? Hakika.

88 Hivyo ndivyo ilivyo hoja.

Sasa, asiyeamini siku zote ata-huenda kwenye kutumia akili, lakini imani haitaligusa hilo! Isingekuwa jambo la maana kwa baba yetu, ambaye ni baba yetu wa imani, Abrahamu-ambaye sisi ni watoto wake, katika Kristo-isingekuwa jambo la maana yule mwanamke wa umri wa miaka sitini na mitano, na angeishi na yote-tangu yeye akiwa msichana-hawangeweza kuwa na mtoto? Na Sara alipokuwa na umri wa miaka mia au tisini, na Abrahamu miaka mia, na bado bila mtoto. Je, usingewazia... Baadhi ya kundi la madaktari na wanasayansi wakuu walimchunguza Sara na kusema, "Mbona, tumbo lake la uzazi limekauka. Mishipa ya maziwa ilikauka miaka arobaini iliyopita." Moyo wake kwenye ule umri-yeye hangeweza kwenda kwenye utungu wa kuzaa. Mbona ni jambo lililo wazi tu. Lakini Abrahamu alilikataa! Yeye hakuyumba kwenye ahadi ya Mungu kwa njia ya kutokuamini dhidi ya ufahamu wa kiakili-yeye hakuyumba kwenye ahadi ya Mungu, haidhuru ilikuwa ni nini, kwani yeye alikuwa amemhesabu Mungu kuwa anaweza kufanya kila kitu ambacho Yeye alisema angekifanya.

89 Sasa, watoto wa Abrahamu wako wapi asubuhi hii? Ninyi wahudumu mnaoogopa kuwa... mnaogopa juu ya mkate wenu na maji yenu... barabarani kama mtaondoka kwenye hiyo Babeli; imani yako iko wapi? Daudi alisema, "Nalikuwa kijana, na sasa ni mzee; sikuwahi kuona mwenye haki aliyeachwa au uzao Wake ukiomba mkate." Usiogope. Udumu kuwa mwaminifu kwa Kristo.

90 Lakini kutokuamini kulidaka hoja. Hicho ndicho lilichofanya... Sasa, unalipata? Kutokuamini kunategemea hoja-jambo la leo. Imani haiwezi kufanya hilo. Imani hutazama Neno, lakini imani hujiweka yenyewe juu ya mwamba usiotikisika-Neno la Mungu la Milele. Amina! Imani haitazami hoja. Sijali ni kiasi gani unaweza kuonyesha ingekuwa bora, kama Neno linaserna, "Hapana," imani hutulia pale. Hapo ni mahali patakatifu pa mapumziko pa imani.

91 Nataka niwaulize, Lutheran, asubuhi hii; ninyi Wababtisti, na ninyi Wakatoliki, na ninyi, yeyote awaye-ninyi watu wakidhehebu ulimwenguni kote: Jinsi gani mnaweza kuweka imani yenu juu ya dhehebu lenu wakati lipo kinyume na Neno? Ni imani ya jinsi gani mliyo nayo? Mnayo hoja ya nguvu na siyo imani. "Kwani imani huja kwa kusikia," kusikia baraza La umoja wa madhehebu? Mngeweza kusema... Mnaweza kupata hilo katika Ladies Day Almanac, lakini kamwe huwezi kulipata katika Neno la Mungu.

92 "Imani huja kwa kusikia, na kusikia huja kwa Neno la Mungu." Amina!

Niambie yule mtu mmoja awezaye kusema chochote kinyume na hilo na kusema ni Neno la Mungu, wakati mbingu na nchi zitapita lakini Neno halitapita. Imani hulipata Neno, mahali pake patakatifu, pumziko. Inatembea moja kwa moja juu ya kilele cha Mwamba wa Milele, Kristo Yesu, Neno, na kukaa pale chini na kupumzika.

Pepo na zivume; dhoruba zitingishe; Bibiarusi yu salama daima. Yeye anatulia pale pale kwenye lile Neno. Hapo ndipo imani, imani halisi ya Mkristo inapotulia. Mahali pa kupumzika ni Neno. Kwani inajua kuwa Mungu atajithibitisha Yeye Mwenyewe kuwa mwenye uwezo zaidi ya kila mmoja wa maadui Zake. Haidhuru inaonekana ni mbaya jinsi gani, au jinsi gani maadui wanaingia; jinsi gani inaonekana kama umeshindwa, imani bado inajua.

93 Sasa, kwenu ninyi watu wagonjwa, ee, jinsi gani ningependa kulileta hili lifike mahali pake. Unaidaka ile imani kuwa unakwenda kuponywa, kila-kila hali, chochote kile, kila ishara, kila dalili zaweza kuelekeza kuwa unakufa, kamwe hutatikisika.

Mahali pake pa kupumzikia ni katika patakatifu pa Neno la Mungu, wakati imani, imani halisi inajiweka yenyewe pale. Siyo imani ya kujifanya sasa-imani. Siyo tumaini-bali imani; Tumaini liko nje *hapa* likitumaini lilikuwa ndani. Imani tayari iko ndani, ikitazama nje na kusema, "Imekwishatendeka." Hiyo ni imani! Hapo ndipo imani inachukua mahali pake pa kupumzikia, kwani inajua kuwa Mungu kamwe, kamwe hamwachilii adui atembee juu yake. Kamwe hajawahi kuachilia. Imani inajua hilo, kwa hiyo bila kujali kile kitu kinaonekanaje...

Nuhu alijua ile safina ingeelea-hakika alijua. Danieli alijua kuwa Mungu angeweza kufunga kinywa cha simba! Wale wana wa Kiebrania walijua kuwa Mungu angeweza kuuzima moto!

94 Yesu alijua kuwa Mungu angemfufua Yeye tena, kwa sababu Neno lilisema, "Sitaacha nafsi Yake katika Kuzimu, wala sitaacha Mtakatifu wangu aone uharibifu. " Yeye alijua uharibifu wa mwili unakuwa katika masaa sabini na mawili, na Yeye akasema, "Katika siku tatu nitafufuka."

Unaona, ilichukua mahali pake pa kutulia pa Milele katika mahali patakatifu pa Neno la Mungu, na pale limesimama.

95 Hoja itajaribu iwezavyo kutambua ... Vema, "*Huu* mfumo hauna budi kuwa bora. *Huu* ndio ule." Linaonekana bora kwa sababu unatazama kwa mawazo ya kiakili. Unaweza kuthibitisha fikira. Lakini huwezi kuthibitisha imani, kwa sababu kama ungeweza kuithibitisha, haiwi imani tena. Lakini imani inajua Neno na ahadi pekee, na inatazama lile jambo ambalo hulioni. " ... imani ni hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Huwezi kutoa hoja, siwezi kuthibitisha jinsi itakavyofanyika sijui jinsi linavyokwenda kufanyika. Mimi sijui, lakini naliamini. Najua kuwa ni hivyo, kwa sababu Mungu alisema hivyo, na hilo linamaliza. Hiyo ndiyo sababu najua kuwa Hili ni sahihi.

Najua Neno ni sahihi! Najua Ujumbe ni sahihi! Kwani upo katika Neno, na namwona Mungu aliye hai akitembea miongoni Mwake kulithibitisha Hilo!

Tuko kwenye kutoka, kweli kabisa.

96 Hata kifo chenyewe hakiwezi kuitikisa imani. Mtu anaweza kusimama moja kwa moja katika ... kifo-moja kwa moja katika kukabili kifo na kushangilia ushindi wa ufufuo.

Paulo ... "Ee, kifo ku wapi uchungu wako, kaburi uko wapi ushindi wako?" kwa sababu Kristo alifufuka, na wale walio ndani ya Kristo watakuja Naye kwenye kuja Kwake. Unaona-haliwezi kubadilika. Ndiyo.

Imani hufanya Neno la Mungu pake pa kupumzikia milele. Inakaa katika Neno la Mungu.

Tazama tena...

97 Sasa tumeendelea na somo hili zaidi kidogo, kwenye dakika ishirini na tano, kama hamtajali. [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Nataka kuendeleza hii kanda kwa dakika moja.

Tazama, mfalme, yule mfalme mpya aliyeinuka ambaye hakumjua Yusufu-mpango wake wa kwanza wa kuangamiza nguvu ya Israeli ilikuwa nini?-Ulikuwa ni kwa watoto wao. Hiyo ni sahihi? Yeye alijaribu kuangamiza watoto wao. Sasa, sikiliza kwa makini.

Shetani yule yule katika umbo tofauti la kifalme alijaribu kumwangamiza Mwana pekee wa Mungu. Unaona, kuondolea mbali watoto kwanza, kabla hawajaanza. Shetani ni ndege mjanja na mwerevu. Anajua jinsi ya kugonga jambo kabla halijaanza; analijua hilo, unaona. Na jambo pekee unaloweza kufanya umshinde ni kumtegemea Kristo, ni ujinyenyekeze mwenyewe na umwachie Yeyc akuongoze. Kamwe hutalifanya kwa namna nyingine yoyote.

Nguvu zako za kiakili kamwe hazitalifanya. Unapaswa uliamini hilo na umtumaini Yeye. Yeye ni Mchungaji. Sio kazi ya kondoo kufukuza mbweha, ni kazi ya Mchungaji lakini kondoo lazima wakae na Mchungaji ili kwamba wawe salama. Hilo ni eneo langu la usalarna, ni ndani ya Kristo, na Kristo ni Neno. Hilo ndilo eneo la usalama.

98 Tazama, Ibilisi katika umbo la Ramisesi, mfalme. Jambo la kwanza alilofanya ni kuwaondolea mbali watoto kwa kifo cha asili, na mara tu baada ya kuzaliwa Mwana wa Mungu, huyu alitoka Misri; kwa sababu Mungu aliangamiza Misri. Akailaani, na haijawahi tena kurejea hali yake tangu hapo.

Ndipo akawa Rumi. Shetani alihamisha kiti chake hadi Rumi. Na jambo la kwanza Rumi ilichofanya ili kuangamiza jambo lote, ili kuwa na hakika... Shetani katika ule mfumo wa Kirumi alijaribu kuharibu nini?-Mwana wa Mungu kwa kuanzia, Shetani yule yule.

Na leo yeye amefanya jambo lile lile, chini ya ishara ya roho, sasa, akiwa wa kidini, akikiri Ukristo, na kuchukua wasichana wetu na kuwaoza kwa wavulana Wakatoliki na kuwafanya wawalee watoto wao katika itikadi ya Kikatoliki ili kuvunja nguvu ya ule upande mwingine. Hilo ndilo pepo lenu. Huyo ndiye Shetani wenu aliyeketi juu ya vilima Saba, akiwa amevaa taji za utatu. Akiwa tu mwenye hila, mwerevu, wa kisasa na mwenye akili nyingi kama yule nyoka, uzao wa nyoka-watoto wake. Akitumia mbinu zile zile za kiakili.

Tazama.

99 Ndipo waliua watoto katika hizo nyakati nyingine mbili. Waliua watoto kwa kitu gani? Mara mbili... sasa kumbuka, tazama zile mbili na zile tatu, unaona. Yeye aliwaua watoto mara mbili za kwanza kwa kifo cha asili. Na huu wakati wa mwisho, anachukua watoto na kuwaua kwa kifo cha kiroho-katika kuoa, kujichanganya na madhehebu mengine kwa kuoana.

Je, Danieli hakusema jambo lile lile katika huu ufalme wa chuma na udongo, kuwa wangechanganya mbegu zao kujaribu kuvunja nguvu ya hao watu wengine, na hilo ndilo wanalolifanya? Hadi wapate kile kitu sasa-wao wamemwingiza madarakani rais aliyetoka kwao; sasa jambo linalofuata mpasalo kufanya ni kumweka kadinali madarakani. Watawaweka madarakani baraza lote la mawaziri lililotokana na wao, basi mtakwenda kufanya nini?

100 Jambo linalofuata watakalofanya, wanachukua fedha zao na kulipa deni la Marekani, na kukopa kutoka kanisa na ndipo mtakapokuwa mmeuzwa. Sasa, tuna-tunaishi leo, tukilipa deni letu la nje kule kwa fedha za kodi ambalo haliwezi kwisha hadi ipite miaka arobaini. Sisi hatuna fedha tena, lakini kanisa linazo. Je, Biblia haisemi kuwa yeye amepambwa kwa dhahabu na... ee jamani... lakini…Hivyo ndivyo linavyofanya, unaona.

Wataoa mabinti wenu; mabinti wenu wataolewa na wana wenu, watawalea watoto Kikatoliki, kabisa-linawaua kwa kifo cha kiroho. Je, Biblia haikusema kuwa yeye angemtupa huyu katika kitanda cha kiulimwengu na kuwaua watoto wake kwa kifo cha kiroho-Ufunuo 17. Unaona?

Siku zote ni Neno. Sijali unakwenda wapi, bado ni Neno. Inabidi lilingane moja kwa moja katika ile sura, kama halilingani, sio Neno, sio Neno. Kama huwezi kulifanya

likubalike kote katika Biblia, basi ni kosa.

101 Tazama. wakati huo, Mungu alikuwa anamfundisha mtumishi Wake kwa ajili ya kazi Yake. Akimfundisha mbali nao, nje ya mipango yao, taratibu zao. (Unalipata hilo?) Nje ya mpango wao wa shirika la dini, Mungu alikuwa anamfundisha mtu kwa ajili ya kusudi Lake. Yeye alikuwa analiachilia tu liendelee.

Alimruhusu akaoa na kuwa na mke wake na watoto, mtoto, Gershon. Anaishi maisha mazuri, akimbariki nje kule. Lakini wakati wote alikuwa anamtayarisha kwa kumpa mafunzo.

102 Mungu, na adui Wake walifanya katika asili wakati ule, kama tu Mungu na adui Wake anavyofanya katika kiroho sasa.

Wanawaua kwa kifo cha asili, sasa kwa kifo cha kiroho, unaona. Mungu alikuwa anamtayarisha mtu wa asili, nabii Wake, kwenda chini katika Misri. Na Shetani alikuwa anamtayarisha Ramisesi, mtu wake wa asili, unaona-akimtayarisha mtu wa asili. Nini?-kuua au -kuwaunganisha Wamisri na Waebrania wote pamoja na kuwafanya watumishi wa Farao.

Hiyo ndiyo sababu ni vigumu mno kwa akili kuwaza dhidi ya mfumo wa kielimu ambao unaweza kuthibitisha hoja zake. Hilo ni sahihi, akili siku zote itakwenda kwenye elimu. Wenye akili nyingi na akili za kuwazia hoja hata hawalioni hilo.

103 Je, mliona filamu ya "*Amri Kumi*" ya Cecil DeMille? Nadhani wengi wenu mliona. Siamini katika kwenda kwenye maonyesho ya sinema na mambo haya yote, lakini napendekeza filamu hiyo kwa kanisa kuwa mtu yeyote... kama hawakuwa na lolote ila hilo, wale waliotaka kuiona. Ingekuwa vema kama walitaka kuiona, kwa sababu singemruhusu... Kwanza, baadhi ya ndugu zangu walikwenda; wakaja wakiniambia, sikuwahi kuwa mahali penye maonyesho ya filamu kwa miaka mingi, na hatimaye, nilikwenda chini kule, wakati ilipokuwa kwenye ua wa maonyesho ya sinema, na nikaitazama. Na nikaiona ilikuwa ni kitu gani, na ndipo, nikaliambia Kanisa, "Kama mnataka kwenda kuona ile, ni vema."

Ilikuwa kule. IIikuwa inapendeza, nzuri.

104 Ama kweli hila ya Shetani, jinsi alivyokuwa mdanganyifu ndani pale. Jinsi alivyoingia pale kuwaua wale watoto, jinsi akili za Kisomi zilivyolipokea hilo na kuliamini kwa sababu waliweza kuliona, na lilikuwa linaridhisha.

Ee, jinsi Mungu alivyokuwa akimpa mafunzo huyu nabii wakati wote; na jinsi Misri ilivyokuwa ikimpa mafunzo ya siasa Ramisesi, achukue madaraka. Na ndipo shindano kuu likaja siku moja kati ya wenye akili nyingi na nguvu za kiroho. Na Ramisesi pamoja na miungu wake wote-na akisimama pale na kumwaga maji ndani kumtukuza mungu wa mto Nile. Mungu akampiga, na damu ikaruka kutoka ndani mwake. Ee, nilidhani ilikuwa inastaajabisha, unaona, kuona kile kilichotokea.

Loo!

105 Sasa, tazama, wenye akili nyingi siku zote wata-huenda kwenye kutoa hoja, na hawawezi kuona upande wa kiroho kwa sababu ni wa kiakili. Ee, wala wakati mwingine wowote hawakuwahi kuliona, hawawezi kuliona sasa.

Hawakuweza kuliona hilo katika siku za Eliya, jinsi gani huyu nabii mmoja mzee mwenye uso uliotuna… Mungu nisamehe kwa kusema jambo kama hilo, lakini nafanya tu ... Mungu anajua najaribu kufanya-kufanya hilo liwe lipasalo kudhihakiwa kadiri niwezavyo, ili kwamba mmweze kumwona Roho wa Mungu. Kama Paulo alivyosema, "Kamwe sikuja kwenu nikinena maneno ya kushawishi na hekima, kwani nia zenu zingechukuliwa na hekima; lakini nimekuja na nguvu za Roho Mtakatifu aliyeko hapa, kwamba taraja lenu na tumaini lingetulia, sio katika hekima ya mwanadamu, ila katika nguvu za ufufuo wa Yesu Kristo."

106 Hiyo ndiyo sababu nalifanya hili la mzaha mno kwa kumwita nabii mkuu wa Kiungu mwenye uso uliotuna, kwa sababu angeweza kuwa alikuwa anaonekana kitu cha kutisha kusimama pembeni mwa kasisi aliyevaa vizuri, na ajiite mwenyewe mtu wa Mungu. Mtazame; ungeweza kuona utakatifu wa yule kasisi katika akili za kisomi.

Ungeweza kuona kilemba kichwani mwake na ilivyogeuzwa upande ... na naivera ikiwa imelala kifuani mwake hapa. Ungeweza kuona mafuta ya upako, (ya asili) juu ya ndevu zake yakitiririka chini kwenye pindo za vazi lake. Ungeweza kuona mioto ya

dhabihu ikiunguza na matambiko yote yakiwa katika utaratibu.

Sasa, hilo ndilo ile akili ya asili ingeliendea. Hilo ndilo wao wanajaribu kufanya leo. Jicho, lango la kuingia nafsi, lakini unaona, jicho la kiroho nyuma ndani ya lile jicho. Walimtazama huyu mtu mzee umbo la kujifumba akiwa amesimama pale, akiwa na nywele kifuani mwake na kipande kikubwa cha ngozi ya kondoo akiwa amezungushiwa ngozi, mshipi kiunoni mwake na... labda miguu mitupu na mikono midogo midhaifu iliyokonda, na nyama zikining'inia chini namna hii, na ndevu nyeupe zikitiririka kote usoni pake, na mkwaju mkononi mwake, akiwa amesimama pale, lakini jicho la kiroho lingeweza kuona nguvu za Mungu zikitembea pale, kwa sababu alikuwa pamoja na-Neno kabisa.

Sio kile inachoona akili nyingi; kile jicho la kiroho linachoona.

107 Na jicho la asili, leo, huona kanisa lenye uzuri wa kudanganya, ushirika na meya wa jiji au zaidi-katika haya madhehebu, shirika la dini, na wanashindwa kuona nguvu za Roho Mtakatifu wakati Yeye anapofufua wafu na kuponya wagonjwa na... na jinsi, unaona... wanatazama... Wanatazama sinema za kiulimwengu za Hollywood, na wanatazama watu barabarani.

Wanawake leo hudhani. "Mbona, huyu mwanamke, Suzy, yeye ni wa kanisa. Nywele zake zimekatwa. Anavaa mapambo. Kila mtu mjini anampenda." Sijui kuhusu Mbinguni. Wakati ni kinyume na Neno, Mungu hawezi kuridhia hilo. Hata kama... Angeridhia hilo dhidi Yake Mwenyewe, Yeye angekuwa analikana Neno Lake Mwenyewe, na ijulikane, Mungu kamwe hatafanya hilo! Ijapokuwa mbingu na nchi zitapita, mwanamke aliyekata nywele ni laana mbele za Mungu, au mwanamke ambaye atavaa vazi linalompasa mwanamume.

Ona, jicho la kiroho linalidaka hilo. Wanaishi kwa ajili ya baadaye. Akili za asili hukaa zikiwaza mambo ya kimwili ya ile siku.

108 Tazama, sasa Mungu akitenda hili na bado, watu hawakulijua. Akili za kimwili zilikuwa zinakwenda pamoja na kufikiri. Mungu sasa anaagiza kutoka kwa kiroho. Pale Yeye alipoita kutoka kwa asili kwa ajili ya watu Wake, Yeye anaita kutoka kiroho leo-kwa nani wake?-Wateule Wake. Kwa wateule Wake pekee!

109 Sasa, Misri isingeweza kuona Israeli wakiwa sahihi. Ijapokuwa ile damu ya mwanakondoo juu ya mlango na miimo na yale mambo yaliyokuwa yakitukia. Na Mungu chini kule, akitembea ndani ya nabii Wake na kuchukua neno la mwanadamu.

Hebu yeye asimame juu kule na achukue fimbo kama ile aliyokuwa akiegemea na aielekeze mashariki na kusema, "Na waje nzi na wavamie Wamisri."

Akatembea nyuma kule. Na kila mtu akasema, "Hakuna kitakachotokea. Hakuna kilichotokea." Lakini kwa kitambo kidogo tu, nzi wa kijani wa kale lazima awe alianza kuzungukazunguka pale. Baada ya kitambo kidogo, kulikuwa na labda ratili mbili kwenye yadi moja ya mraba, kwamba mtu alinena uumbaji ukawepo.

Hapa kulikuwa na Ramisesi mwenye akili nyingi akiwa amesimama pale. Hilo Iilikuwa kinyume… mtu wa kidini mno na kinyume na Roho wa Mungu aliye Hai. Na akili za asili zingeweza tu kumwona Ramisesi, lakini akili za kiroho ziliona ile Ahadi, na kuona Hiyo ikitukia.

110 "Vema, kama Joshua na Kalebi wangeweza kuwaita wale Waamaleki na Wahivi, na Wayebusi, kama vile hawakuwepo kule, walikuwa na umbo mara mbili yao au mara tatu au mara nne, na mtu wa asili pale Kadeshi Barnea wakati wapelelezi na wale wengine waliposema, "A-a-ah, hatuwezi kufanya hilo. Wametuzidi mno! Mbona tuko kama, tuko kama panzi pembeni mwao." Lakini Kalebi na Joshua waliona ahadi ya Mungu, wakasema, "Tunaweza kufanya hilo na zaidi." Mbona, walikuwa wanatazama- Mungu alisema, Nitawapa ile nchi," unaona.

Akili za kimwili hazipati hilo. Akili za kiroho hulichukua hilo.

111 Na mbona... Ninapenda kuwauliza jambo fulani. Kwa nini Wamisri hawakuona mambo haya? Kwa sababu hawakuwa wamechaguliwa.

Mungu alimwambia Abrahamu kabla halijatokea ... (Lichukue hilo, wewe Kanisa Mungu alimwambia Abrahamu kabla halijatokea… (Lichukue hilo, wewe Kanisa lililolala!) Mungu alimwambia Abrahamu kabla halijatokea. "Uzao wako utakaa Misri kwa miaka 400, nami nitawatoa nje." Hiyo ndiyo sababu wao waliona hilo, kwa sababu

walichaguliwa walione hilo-wao walichaguliwa.

Israeli ilichaguliwa ili waone ishara ya Mungu, nao walitoka Misri ambapo wasioamini waliangamia! Na leo, Mungu anaita wateule Wake, Uzao wa Kiroho wa Abrahamu kwa imani ile aliyokuwa nayo katika Neno la Mungu.

Je, huoni ule Uzao wa kiroho leo? Ule hauoni kanisa la akili nyingi, unaona Neno. Na umeitwa toka kwenye yale madhehebu makubwa kuingia katika Yesu Kristo. Hilo lilikuwa linaeleweka? Mlilipata hilo? Vema. Tutaendelea mbele kidogo.

Wateule pekee! Daktari D.L. Ph. Kamwe hawajawahi kuona hilo. HawakuchaguIiwa.

112 Na kumbuka, huu uchaguzi unaokuja sasa, hauendi tu kwa taifa Iingine. Unakwenda Utukufuni, pale ambapo majina yao yameandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwaka-Kondoo. Sio chini ya mwanakondoo mdogo wa asili, yule aliyewatoa Israeli, kwamba wangeweza kurudi nyuma toka pale na kurudi, lakini hili haliwezi. Hili liko chini ya Damu ya Mwana-Kondoo wa Mungu, yule aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na majina yao yaliwekwa kwenye kile Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Wako ndani pale, wateule, na ile nuru inapomulika juu yao namna ile, zile kuta za kidhehebu zinadondokea mbali kutoka kwao, na hapa wanakuja... "Tokeni kati yao," asema Roho Mtakatifu katika hizi siku za mwisho. "Msiguse vitu vyao vichafu. Nitakuwa Mungu kwenu; mtakuwa wana na mabinti Kwangu."

Sasa tazama.

113 Israeli ilikuwa inatazama. Walijua kuwa Mungu alishughulika na manabii Wake, wao-lile Neno lilikuja kwao, na wao walikuja kuliona hilo, nao waliliona hilo. Na sasa ishara ya kiakili, tunaliona hilo sasa, kwamba wanaamini juu ya mashirika yao ya dini. Bado wao wako kwenye kanuni zao za imani. Bado wao...

Kama tu alivyokuwa Balaamu, yule aliyekwea juu ya kilima pale Israeli walipokuwa. Kulikuwa na Israeli, sio taifa, watu, wakisambaa huko na huko na walikuwa na hatia! Na Moabu, kaka yake, mwenye akili nyingi, mtu wa shirika Ia dini, alikwea juu ya kilima pamoja na askofu, au nabii waliyekuwa naye na kutengeneza madhabahu na kutoa dhabihu ile ile, lakini yeye alishindwa kuona ile Nguzo ya Moto na Mwamba uliopigwa miongoni mwa Waisraeli.

Ndivyo hivyo leo. Mawazo ya akili nyingi yalikuwa yakitazama mtu maarufu akiwa amesimama pale. Walishindwa kuona Mwamba uliogongwa. Hata askofu mwenyewe alishindwa kuona zile nguvu za Roho Mtakatifu na yowe ya yule Mfalme kambini. Walishindwa kuliona hilo.

114 Kwa hiyo, hiyo ndiyo njia ilivyo tena leo. Mungu anaita. Watu Wake waliochaguliwa, nao wamechaguliwa sasa. Na sasa, wamechaguliwa kwa ajili gani? Kwa ufufuo, na ni ishara ya namna gani Yeye anawaonyesha wao?-ishara ya ufufuo. Yeye alikuwa anawaonyesha nini basi? Ishara ya ukombozi, kuwakomboa toka utumwani. Ishara ya nguvu ile ambayo ingeweza kufunga mbingu au ingeweza kufanya anga liwe giza.

Sasa Yeye anaonyesha nguvu za ufufuo wa Mwana Wake akiishi miongoni mwao kuwafufua wao toka kwenye hili kaburi-na makaburini kule tuliko, kwenda ile nchi Yeye aliyoahidi kwetu-ishara ya Ufufuo-ikiita nje Misri ya kiroho na Babeli ya kiroho.

115 Kwa kujua, hebu mimi niseme hili, kwa taratibu sasa, kwamba mtalidaka hilo. Kwa kulifanya hilo kwa mfumo ule ule ambao Yeye alifanya pale mwanzo, jambo lile lile- Yeye anafanya, akipofusha macho ya asiyeamini, akifungua macho ya mwaninio. Na tazama, siasa zinalifanya hilo kwenye upande wa akili nyingi, siasa na siasa za kanisa na mataifa, kila kitu na ule upande mwingine ni-limefichwa toka kwao, kesi ya kiroho.

116 Mungu alimpeleka mtu mmoja kule jangwani, akampa mafunzo na kumrejesha, na kuchukua kile kitu kule na akatoa wale watu nje. Unaona, kile ninachomaanisha? Yeye hawezi kubadilisha utaratibu Wake. Yeye ni Mungu. Kamwe hatashughulika na kundi; kamwe hajawahi kufanya hivyo; Yeye anashughulika na mtu binafsi, na Yeye alifanya hilo, na Yeye atafanya hilo, na Yeye aliahidi hata katika Malaki 4, Yeye atafanya hilo. Hilo ni sahihi.

Kwa hiyo, hiyo hapo ahadi Yake kile Yeye alichokuwa, aliahidi kile Yeye alichosema Yeye angefanya, na hapa tumefika! Watu wa jinsi gani, tungekuwa na furaha-akiwapa wao ile ishara kwa Neno lililoahidiwa. Yeye aliahidi angefanya hilo. Na Yeye atarejesha

ile imani ya watu, mioyo ya watu irudi kwenye imani ya wale mababa wa asili wa Kipentekoste. Yeye aliahidi kufanya hilo, akionyesha ishara Zake.

Na, "kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa kwenye kuja kwa Mwana adamu." Ni ishara ya namna gani makanisa yaliona kule Sodoma? Kanisa la kiakili liliona nini?-wahubiri wawili. Nini Kanisa la kiroho, lililochaguliwa, Abrahamu na kundi lake?-waliona Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa nyama, wa mwili wa mwanadamu, ambaye aliweza kutambua roho na kusema kile Sara alichokuwa akisema nyuma Yake.

"Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana adamu." Tunamwona Roho Mtakatifu miongoni mwetu akitenda jambo lile lile, akitenda katika mwili wa mwanadamu. Hii ndiyo sasa ile, unaona. Tuko tu hapa, marafiki, hivyo tu. Kutoka kunaendelea.

117 Lakini sasa, tazama, Yeye alilifanya hilo wakati ule kwa kutumia nini? Tazama na uliweke kwenye kufikiri kwako kiroho. Roho Mtakatifu na aweke nyuma kifuniko cha zamani cha kutojali sasa, na utazame kwa makini. Mungu anapoamua kufanya chochote kwa njia moja, Yeye kamwe hawezi kuibadilisha hiyo.

Katika Bustani ya Edeni, wakati Yeye alipotaka kumkomboa mwanadamu na kumrudisha kwenye ushirika, Alifanya uamuzi, ilikuwa ni Damu. Wamejaribu elimu, wamejaribu dhehebu, wamejaribu kufanya kuwa mali ya taifa, na kila kitu kingine, na kamwe halikufanya kazi.

Kuna mahali pamoja pekee ambapo Mungu daima hukutana na mwandamu, hapo ni chini ya Damu iliyomwagika, kama ilivyokuwa katika Edeni. Haijawahi kubadilika kamwe. Mahali pekee alipokutana katika siku za Ayubu ilikuwa chini ya mwanakondoo wa kidhabihu. Mahali pekee Yeye alipokutana katika siku za Israeli, chini ya mwanakondoo wa kidhabihu, kama Alivyofanya katika Bustani ya Edeni, chini ya mwanakondoo wa kidhabihu.

Mahali pekee Yeye anapokutana leo siyo katika madhehebu-wanaudhiana na kuchokozana mmoja kwa mwingine siyo katika kule kuwa mshirika wa kanisa-bado wanafanya jambo lile lile; siyo katika wasomi-wote wamechanganyikiwa, lakini chini ya Damu ya Mwana-Kondoo; kila mwaminio anaweza kukutana na ushirika, pale Uzima ulipo.

118 Mungu alichagua katika siku za kutoka, Yeye alitoa nje kundi na kutoka kwenye lile kundi ... Nataka muwone jambo fulani. Yeye alikuwa na wawili pekee, wale waliokwenda kwenye Nchi ya Ahadi. Yeye alichagua nini cha kuwatoa nje? Siasa? Shirika la dini? Alichagua nabii mwenye ishara ya Kiungu ya Nguzo ya Moto, kwamba watu wasingelikosea. Kile yule nabii alichosema kilikuwa Ukweli. Mungu alishuka chini katika Nguzo ya Moto na-kujidhihirisha Mwenyewe, alionyesha Neno Lake, Hilo ni sahihi?

Hicho ndicho Yeye alileta-kutoka Kwake kwa kwanza. Kutoka Kwake kwa pili... Yeye ni mkamilifu katika tatu. Ninyi nyote mnaona kuhubiri kwangu, siku zote ni tatu na saba. *Saba* ni kumaliza; *tatu* ni ukamilifu Wake. Mvuto wa Kwanza, wa Pili na wa Tatu na o-o-oh na kuendelea na kuendelea-kila kitu, unaona. Kuhesabiwa haki, utakaso, Ubatizo wa Roho Mtakatifu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, kila kitu.

Angalia.

119 Yeye alifanya nini, kule kutoka kwa kwanza? Yeye alituma nabii, mwenye upako wa Nguzo ya Moto, Naye aliwaita watu nje. Hiyo ilikuwa kutoka Kwake kwa kwanza. Na ule wakati wa Israeli ulikuwa umefika, Alituma tena Nabii-Mungu, akiwa na nguzo ya Moto. Yohana aliiona ikishuka kutoka Mbinguni kama hua. Na yeye akasema, "Nakwenda kwa Mungu, na narudi kwa Mungu."

Baada ya kufa Kwake, kuzikwa, na kufufuka, Sauli wa Taso, akiwa njiani mwake kwenda Dameski, aliona ile ile Nguzo ya Moto. Na yeye akiwa Mwebrania, aliyefundishwa vyema katika Neno, akasema, "Bwana Wewe ni Nani?"

Yeye alijua ilikuwa Bwana, ile Nguzo ya Moto. Yeye alikuwa Mwebrania. Akasema, "Wewe ni Nani?"

Na Yeye akasema, "Mimi ni Yesu."

120 Kutoka kwa pili, Yeye alileta nabii aliyepakwa mafuta, ambaye alikuwa Mwana Wake, Nabii-Mungu. Musa alisema Yeye angekuwa nabii, na alikuwa na Nguzo ya Moto

na alifanya ishara na maajabu, na yule yule nabii alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, naye atazifanya pia."

Na hapa Yeye aliahidi jambo lile lile lililokuwa katika kutoka kutokea katika siku za mwisho, na Yeye hawezi kulibadilisha. Kwa uthibitisho wa kisayansi, kwa ushahidi wa Roho, kwa matendo ya yule Roho, tunaliona hilo leo, ile Nguzo kuu ya Moto ikitembea miongoni mwetu. Na zile ishara na maajabu ya ufufuo wa Yesu Kristo ukiita watu kutoka kwenye udhehebu na kuingia katika uwepo wa Yesu Kristo kuishi- kwenda kwenye nchi.

Hakuna kosa, marafiki; siyo kile ninachosema-mimi ni ndugu yenu tu-lakini ni kile Mungu anachothibitisha kwenu. Hilo linakifanya kiwe ile Kweli. Ile ile Nguzo ya Moto Yeye aliyoitumia katika nyakati zile mbiIi, Yeye ameileta miongoni mwenu leo na kuihakikisha hiyo kisayansi.

Kama mjuavyo, gazeti la Life liliiweka katika toleo lao mwezi uliopita, pale ...

121 Ni wangapi waIikuwa hapa na kusikia mimi nikisema kuhusu kile kingetukia kabla hilo halijatendeka? Nafikiri kuhusu kila mmoja katika kanisa. Ndilo hilo. Wao hawajui hilo lote linahusu nini. Wanasayansi wanajaribu... "Yeyote mwenye picha yake, aje"- wingu la maili ishirini na sita kwenda juu katika sura ya piramidi-Malaika saba waliwakilishwa ndani pale na wakaleta... na walikuletea wewe Neno la Mungu, chini ya uvuvio, na Linawaambia ninyi juu ya saa hizi mnazozijia na kuishi ndani yake. Akili za kiroho zitachukua hilo sasa hivi na kulidaka. Ni kutoka! Tunakwenda kuondoka mojawapo ya siku hizi. Mungu na ashukuriwe. Kumbukeni. Sasa nitamaliza katika muda mfupi ujao. Nina dakika kumi.

122 Tazama, ile Nguzo ya Moto ile iliyowaita wale nje, iliwaongoza kwenda nchi ya ahadi chini ya upako wa nabii. Nguzo ya Moto ambayo waliitazama, iliwaongoza kwenda katika nchi ya ahadi chini ya nabii aliyepakwa mafuta. Na mara kwa mara walimkataa. Hilo ni sahihi? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh] Hakika.

Sasa, najua mnapaswa kuwa na ibada ya ubatizo. Ninazo kwenye kurasa sita zaidi hapa, nadhani, lakini ninakwenda kumaliza sasa katika muda mfupi tu.

Litazame, tuko katika kuitwa nje. "Tokeni Babeli, watu wangu," ikasema sauti ya Malaika. Nje ya nini?-machafuko.

Je Methodisti liko sahihi? Au Babtisti? Au Katoliki? Tokeni kwake! Mungu yuko sahihi. Unajuaje? "Hebu kila neno 1a mwanadamu liwe uwongo na Langu Ukweli." Tokeni kwake. Unajua kitu gani? Ile ile Nguzo ya Moto, Roho yule yule wa atiaye mafuta, akiongoza kwenda nchi ya ahadi. Tazama, aliwaongoza, aliwatoa nje, akawaongoza kwenda nchi ya ahadi, Israeli, lile taifa.

123 Na Mungu yule yule, Nguzo ya Moto ile ile; ile pekee... Wanasema, ile ... ile kamera ... Unaposoma ile ya Gerge J.Lacy... sio mimi sasa-usome pale Gerge J.Lacy alipoichunguza ile picha (yule mkuu wa F.B.I. kwa ajili ya hati za alama za vidole) pale kuna taarifa yake. Baadhi yao husema, "Lensi iliyopiga picha mara mbili."

Makumi ya maelfu ya watu waliiangalia kwa macho yao wenyewe. Tulisimama hapa na kuitazama; ninyi mmeitazama. Siyo! Walisema ilikuwa ni mauzauza ya Iensi. Bwana Lacy alisema nini? Jicho la hii kamera haliwezi kupiga picha ya saikolojia."

Haikuwa mauzauza ya Iensi; ilikuwa pale-ile ile Nguzo ya Moto. Ndipo wanasema, "Ee, vema, hiyo ilikuwa mauzauza." Sasa, kamera zote-kwani katika mamia ya maili toka Tucson.

124 Miezi sita kabia halijatukia, tuliwaambia ninyi kwa Roho Mtakatifu, ningekwenda kule kuchukua habari za matukio. Kwa sababu kuandikwa kwa piramidi kwa nje... kama ndugu alivyoota ndoto na nikawafasiria ninyi. Hiyo ndiyo fasiri yote.

Sasa, Mafumbo yote ya kuhesabiwa haki, utakaso, Ubatizo wa Roho Mtakatifu yamekwishaeIezwa. Sasa, tukichukua miisho iliyoachwa ya ile ambayo ilifichika katika ile Mihuri Saba; siyo yale Makanisa Saba, ile Mihuri Saba ilifunua yale Mafumbo. Na ndipo Yeye akafungua hili jambo pale juu na kukuta mwamba ndani pale, mweupe, Iakini haukuwahi kuandikcwa juu, ni Fumbo.

Nenda Tucson, tabiri hilo kabla halijatukia. Simama kaskazini mwa Tucson, (mashahidi wakiwa wamesimama hapa pamoja nalo) wakati mlipuko-ulipokuja nusura utingishe milima ing'oke. Na wakati ule ule, duara ya nuru ikining'inia pale angani. Wakati wanasayansi walipopiga picha sasa, maili ishirini na sita kwenda juu, kwenye

umbali mara tano ya ukungu au chochote kile kingeweza kuwa; na wao hawawezi kujua hata kile kilichofanya hilo. "Kutakuweko nuru wakati wa jioni, Njia ya Utukufu hakika mtaipata."

Kama wewe umechaguliwa; ile Mbegu inaanguka juu ya udongo mkavu au juu ya miamba, kamwe haitafanya chochote. Migumu, mioyo ya jiwe inayotaka kuwa na kutojali, lakini kama ikianguka juu ya ardhi nzuri iliyo laini ya imani, itazaa Mkristo, akizaa matunda ya Roho.

125 Tazama, jinsi yule Mungu alivyofanya hilo. Sasa, Yeye anayo ile ile Nguzo ya Moto, ile iliyothibitishwa. Mtu fulani alisema, "Kwa nini usiende kuwaambia wale wanasayansi kuhusu hilo." Unadhani wataliamini hilo? "Usitupe lulu zako mbele ya nguruwe." Yesu alisema tusifanye hivyo; sina maongozi ya kufanya hilo. Bado nikiwa ninaishi hapa hapa katika mji, pale walipokuwa wakitafuta kujua hilo, nilifikiri ningekwenda kule chini, na Roho Mtakatifu akasema, "Kaa mbali, sio kwa ajili yao. Rudi na ukaliambie hekalu."

Vema. Na itatukia… Kama kile wanachosema kitatukia, basi kumbuka, Mimi nimenena," Bwana alisema, unaona. Kabla halijatukia, linatukia pale. Sikiliza Biblia, Ni Sauti ya Mungu ikikuita katika siku hii.

126 Sasa, nataka mmwone, hii hii Nguzo ya Moto inaongoza watu tena kwenda Nchi ya Ahadi, ule utawala wa Miaka Elfu, pale tulipokuta chini ya uvuvio wa huu Muhuri wa Sita, hilo ambalo halikuwahi kamwe kufundishwa kabla, jinsi dunia inabidi itakaswe kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Ile Nguzo ya Moto inawaongoza kwenda kwenye Utawala wa Miaka Elfu.

Na angalia, ile Nguzo ya Moto ile iliyowaongoza Israeli kutoka utumwani katika kule kutoka, ile Nguzo ya Moto, chini ya uongozi wa Mungu, Mungu alikuwa Moto, na Nguzo ya Moto ilimpaka mafuta nabii tu. Ile Nguzo ya Moto ilikuwa isimame kama shahidi wa kimbinguni, kwamba Musa alikuwa ameitwa nje.

Mnakumbuka Dathani na wale wengine walisema, "Vema, tunapaswa kuanzisha shirika la dini. Musa... unajichukulia mengi mno juu yako mwenyewe. Unajaribu kusema wewe ndiyo pekee mtakatifu miongoni mwetu. Kusanyiko lote la Bwana ni takatifu. Jinsi gani unaweza kuchukua hili juu yako mwenyewe?"

Na Musa akaanguka kifudifudi na kuanza kulia. Mungu akasema, "Jitenge mwenyewe na hao. Nitaifungua tu nchi na immeze," Mfano. Jinsi gani Musa- aliwaambia kuwa yeye alikuwa anawaambia kile Mungu alichosema-Mungu akithibitisba kuwa ile ndiyo Kweli.

127 Hata Miriamu, yule nabii mke mwenyewe, na Haruni walimcheka Musa kwa ajili ya kumwoa yule msichana Mkushi, wakimfanyia mzaha; na Mungu akakasirika-kunena dhidi ya mtumishi Wake. Yeye alifanya nini? Aliwaita nje kwenye lango la hekalu, na Miriamu, akiwa nabii mke, lakini Musa alikuwa zaidi ya nabii-zaidi ya nabii.

Yeye akasema, "Je hamwogopi Mungu?" Kukiwepo nabii miongoni mwenu, Mimi, Bwana nitanena naye katika maono na kujijulisha kwake Mimi Mwenyewe katika ndoto." lakini Akasema, "siyo Musa" Akasema. "Je, hamwogopi -Mungu?" Na yeye alikuwa nusu mfu kwa ukoma ile dakika. Mnajua hilo.

128 Je Yeye hakusema, "Yohana Mbatizaji... Mlikwenda nje kuona nabii? Ndiyo, zaidi ya nabii." Kwa nini, kwa nini yeye alikuwa zaidi ya nabii? Yeye alikuwa mjumbe wa Agano-sanduku lile lililochanganya hayo majira mawili pamoja.

Na leo, kile tulicho nacho miongoni mwetu, huyu Roho Mtakatifu mkuu ni zaidi ya nabii. Ni Mungu aliyedhihirishwa miongoni mwetu pamoja na Neno Lake kulithibitisha hilo. Hutenda zaidi ya nabii-mara elfu zaidi ya wanavyofanya manabii.

129 Eliya, mmoja wa manabii wakuu wa kizazi alitenda mambo manne tu ya Kiungu katika maisha yake yote ya kama miaka themanini. Na Elisha akiwa sehemu maradufu alitenda manane. Na tumeona maelfu mara maelfu kwa macho yetu wenyewe! Mtazame Yule Malaika wa Bwana katika Nguzo ya Moto. Uchunguzi wa kisayansi ukaipeleka ulimwenguni, wakijua kuwa wanakwenda kuhukumiwa nayo.

Yule Mwana-Kondoo alifanya nini? Yule Malaika wa Bwana, ambaye alikuwa Kristo. Mnaliamini. [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Mt. Yohana 6, wote walikuwa wanakunywa haya maji na wakiwa na wakati mkuu na kufurahia. Yeye akasema, "Mimi ni Mkate wa Uzima ule utokao kwa Mungu Mbinguni. Mimi ndio ule Mwamba uliokuwa

katika jangwa."

Wakasema, "Sasa tunajua Wewe ni mwendawazimu. Wewe ni mwendawazimu; unaye Shetani juu yako. Wewe ni mtu mwendawazimu wa Shetani." Unajua, watu huwa na roho juu yao, wakati mwingine wanakuwa wa kidini sana.

Wakasema; "Wewe ni, Wewe ni Shetani; unaye Shetani juu yako. Wewe ni Msamaria, na una Ibilisi juu yako." Wakasema, "Na hapa huna hata zaidi ya umri wa miaka hamsini, na unasema umemwona Abrahamu?"

130 "Naweza kumwona Yeye akirudi nyuma hatua kadhaa." Akasema, "Mimi Ndiye. Kabla ya Abrahamu, Mimi Niko." Ule ulikuwa Moto unaowaka, ile Nguzo ya Moto katika kichaka.

Wakati Yeye alipokufa na kufufuka siku ya tatu, na Sauli akakutana Naye njiani chini. Yeye alikuwa amerudi kwenye ile Nguzo ya Moto. Akasema, "Natoka kwa Mungu na Nakwenda kwa Mungu." Petro alipokuwa gerezani, ile Nguzo ya Moto ilikuja ndani na kufungua milango na kumtoa nje. Hilo ni sahihi.

Ile Nguzo ya Moto iliwaongoza kwenda wapi? Sasa, kumbuka, Musa hakuwa ile Nguzo ya Moto. Yeye alikuwa kiongozi aliyepakwa mafuta chini ya ile Nguzo ya Moto, na Nguzo ya Moto ilithibitisha tu Ujumbe wake kwa ishara na maajabu. Na ile Nguzo ya Moto iliwaongoza kwenda nchi ile Mungu aliyowaahidi wao, pale Yeye, Yeye Mwenyewe, angefanyika mwili miongoni mwao siku fulani. Hilo ni sahihi? Walifanya nini? Walijiua na kujinyonganyonga na kila kitu kingine kuonyesha ilikuwa chini ya damu ya mwanakondoo wa kawaida.

Lakini, wakati huu-Utukufu kwa Mungu!-ile Nguzo ya Moto ile tunayoiona miongoni mwetu, ile Nguzo ya Moto itatuongoza kwenye Utawala wa Miaka Elfu, pale Yeye atakaporudi kwa watu Wake katika ule wakati wa kumiliki wa Utawala mkuu wa Miaka Elfu baada ya huku kutoka, pale ambapo tutaishi umilele pamoja Naye. Siku zote yeye ana lile Neno la Baba, siku zote huthibitisha kuwa Hilo ni sahihi.

131 Tuko katika kutoka, na katika kuondoka na kuzima kanda katika muda mfupi, ee, marafiki zangu, ndugu zangu, nyote mliopo hapa na wale watakaosikia kanda, hebu mimi kama ndugu yenu na raia wa ule Ufalme wa Mungu, njooni nje, katika huku kutoka!

Kwani wote wale wanaobaki nyuma watapata Alama ya Mnyama. Tokeni Babeli; tokeni katika haya machafuko; tokeni katika hii mipango na mmtumikie Mungu Aliye Hai. Hebu huyo Malaika mkuu wa Agano, Yesu Kristo, katika hili umbo la Mungu, hakuwaza kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho. Sasa, Yeye ni Nguzo ya Moto katika lile lile umbo ambalo Yeye alikuwa nyuma kule akileta kule kutoka kwa kwanza, akileta kutoka kwa pili, na hapa akiwa na kutoka kwa tatu.

132 Kutoka kwa kwanza, Yeye alifanya nini? Aliwaleta nje toka nchi ya asili kwenda nchi ya asili. Kutoka kwa pili, Yeye aliwaleta nje toka hali ya kiroho kuingia Ubatizo wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Sasa Yeye anawaleta toka Ubatizo wa kiroho wa Roho Mtakatifu, kurudi moja kwa moja kuingia Nchi ya Milele ya Utawala wa Miaka Elfu na ile kuu baada ya hapa. Ile ile Nguzo ya Moto kwa mfumo ule ule wa upako. Mungu yule yule akitenda mambo yale yale. Na Neno lile lile lililomtangaza yule wa kwanza, lilimtangaza yule wa pili. Lile lile Neno lililomtangaza yule wa pili limemtangaza yule wa tatu, na hapa tunaliona miongoni mwetu.

Tokeni! Ee, tokeni nje ya haya machafuko! Njooni kwa Mungu Aliye Hai! Njooni kwenye Neno! "Naye alifanyika mwili akakaa kwetu." Na sasa, Yeye yupo ndani ya miili yetu, akikaa miongoni mwetu. Tokeni nje na mmtumikie Mungu Aliye Hai. Tunapoinamisha vichwa vyetu.

[Unabii unatolewa na mtu fulani katika kusanyiko. "Watu wangu, nitanena nanyi hata katika saa hii. Naam, hata kama ambavyo nimewaambia kupitia huyu nabii leo hii, 'Tokeni kwake watu wangu.' Nawaambieni, Mimi ni Mungu Mwenyenzi. Natazama kutokea kwenye baraza za ghorofani za Mbinguni siku hii. naam, Sauti Yangu imetangazwa miongoni mwenu. Je, mtatoka na kuifuata hiyo Nuru niliyowapa? Kwani nawaambieni, watu wangu, Mimi ni Mungu Mwenyenzi. Neno Langu kamwe halikubadilika. Nimelileta hilo kwenu. Mtalitii? Naam, mtaharakisha katika yote ambayo nimewapa, asema Bwana."]

133 Tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu... kutoka kwenye vilindi vya nafsi zenu, kutoka kwenye vilindi vya yote yaliyomo ndani yenu, mnalikubali kukumbuka ku... mko tayari kuacha mambo yote ya ulimwengu na kuishi kwa ajili ya Mungu. Sasa, kama humaanishi hili, usifanye hilo; lakini kama unalimaanisha, kwa moyo wako wote, kwamba sasa umeshawishika-kama Yesu alivyosema mwishoni mwa huduma Yake, "Sasa je, mnaamini."

Je, umeshawishika kuwa haya mambo ni sahihi, yamethibitishwa na Mungu na tuko kwenye wakati wa mwisho, na kwa kweli unataka kuja kwa Kristo sasa, njoo katika hii kutoka ya kuita nje ya umadhehebu wa kutokujali, mawazo na mambo ya ulimwengu, na unataka kujisalimisha kwa moyo wako wote Kwake na utoke nje katika huku kutoka kwa ajili ya nchi ya ahadi-mtainua mikono yenu tunapoomba? Je, hakika kweli kwamba unataka kutoka nje? Kila mmoja.

134 Baba wa Mbinguni, wale walioinua mikono yao juu, hebu watoke nje sasa, Bwana. Hebu Roho Mtakatifu juu ya Neno la ahadi, hebu Roho Mtakatifu aingie ndani ya mioyo yao. Kutoka kwenye kusanyiko kulikuwa na kama mikono ishirini, nadhani Baba, wale walioridhika na wanajua hilo ni kweli, na wanataka kuja nje.

Kama kulikuwa… Katika siku za kutoka nje kwa Israeli, katika watu milioni mbili na nusu, wawili pekee walifika kwenye ile nchi.

Katika siku za Yesu Kristo, kulikuwa kwenye 120 waliofika.

Na sasa, katika siku za kumalizika kwa ulimwengu, Ulisema, "Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, lakini ni wachache waionao; lakini ni pana iendayo upotevuni, na wengi wataingia humo." Yale maneno hayatashindwa; hayo ni Yako.

135 Sasa, nawaombea hao, Bwana. Naomba kuwa utawatahiri mioyo yao, saa hii, Roho Mtakatifu Wako. Ondoa mambo yote ya ulimwengu. Tahiri masikio yao waweze kusikia kwa dhahiri Sauti ya Mungu, ikiita kwa njia ya Neno Lako na njia ya ile Nuru ya siku hii.

Na jaIia, Bwana, kwamba macho yao yatafunguliwa kwamba wataweza kuona utukufu wa Mungu katika hii saa ya mwisho ya kumalizia. Wewe Ulisema, "Wote wale alionipa Baba watakuja, na nitawafufua siku ya mwisho. "

Bwana, labda wapo wengi hapa ambao bado hawaelewi. Naomba kwamba Utashughulika nao na utawaruhusu kuwa na nafasi nyingine. Bwana, ili waweze kuelewa. Wanakusikia Ukinena kwa njia ya Neno Lako, ukijithibitisha Mwenyewe kunena nasi katika Sauti ya Kiungu, na ndipo kwa fasiri, kuona matendo Yako makuu yakithibitisha hilo kuwa ni kweli kulingana na Biblia.

Naomba, Mungu, kwamba Utasamehe dhambi zetu, sasa. Na ninapolilingana Neno.

136 Mungu, ninawaza kuwa ni wiki moja tu iliyopita, nilijilaza mwenyewe juu ya mtu sakafuni aliyekufa hapa, na nikaona Roho Mtakatifu mkuu akimrudishia uhai. Macho yake yaligeukia upande wa nyuma ya kichwa chake, akiwa amelala pale amekufa na nilipoita Jina Lako kwa maneno machache tu... nilimwona akiwa hai. Yupo hapa leo, akiwa hai bado.

Bwana, Wewe ni yule yule Mungu ambaye Paulo alipojilaza juu ya yule mvulana aliyemsikiliza akihubiri kwa kirefu, yule mtu aliyeanguka dirishani-Wewe ni Mungu yule yule ambaye unaweza kurejesha uhai.

Tunakushukuru, Baba. Hebu… asiyeamini hawezi kuamini, lakini tunaamini, Bwana. Wewe Umejithibitisha kwetu.

137 Sasa, hebu tafakari ya moyo wangu, mawazo ya akili zangu, nguvu zangu, na yote yayeyuke katika hili Neno. Na hebu Neno na mimi, pamoja Bwana, pamoja na watu, tutembee kwenda kwenye Ufalme wa Mungu. Tujalie hilo, Bwana. Tusamehe dhambi zetu, ponya magonjwa yetu, na tufanye raia wa Ufalme Wako.

Na sasa, hawa wanapokuja, Bwana, na kisima kinafunguliwa, maji yapo tayari, na ubatizo utaanza katika dakika chache zijazo, tunakumbuka wakati hii hii Injili ilipohubiriwa, Biblia ilisema, "Wote walioamini walibatizwa."

Hapa kuna leso zikiwa zimekaa hapa, Bwana, ambazo nabariki katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa.

Basi wakati…

138 Ibada zetu zinapokuwa ndefu, mahubiri marefu, kwani masaa yamekwenda- lazima

tuweke Neno ndani hali pana udongo ambao tutaliweka Neno humo, kwani masika ya baridi inakuja. Tunaiona; majani ya miti yanadondoka, na tunajua kuwa masika imewadia. Sharti tuiparue ardhi na kufukia mbegu.

Kwa hiyo, Baba wa Mbinguni, kwamba utanena na kila moyo. Na Biblia ilisema, "Wote walioamini walibatizwa." Na Bwana, kama hakuna... wengi hapa ambao wameamini na hawakuwahi kubatizwa bado, katika Jina la Mwana Wako mpendwa, na waje asubuhi hii, kwa upole na unyenyekevu, wakikiri dhambi zao, na kufa kwa yale mambo ya ulimwengu, wazikwe, walibebe Jina la Yesu Kristo, waishi wakiwa wachaji wa Mungu baada ya hapa kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Tunawakabidhi Kwako sasa, Bwana, kwa kusudi hili, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa, tunarudisha ibada kwa Ndugu Neville, na lolote yeye alilo nalo la kusema tunapojitayarisha kwa ajili ya ibada ya ubatizo. Na usiku huu kwenye saa 1:30, Bwana akipenda, nataka kurekodi huu ujumbe mwingine. Mungu awabariki hadi hapo baadaye.

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

*"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7*